WARAKA
WA
KWANZA
WA
YOHANA

Kimeandikwa na

Dr. William Vinton

GMI publications

1011 Aldon Street, Wyoming, MI 49509, USA
www.vitabuvyakikristo.com

WARAKA WA KWANZA WA YOHANA

Copyright © 2017 GMI Publications

GMI Publications ina haki zote za tafsiri ya kitabu hiki. Hairuhusiwi kuchapa na kuuza sehemu yo yote ya kitabu hiki bila ruhusa ya GMI Publications. Vilevile hairuhusiwi kuuza nakala za kikompyuta (digital copies) bila ruhusa ya GMI Publications.

Mfasiri kutoka Kiswahili cha Congo – Steven Sherman
Wahariri - Mch. Albert Juliano Simwanza, Martin Haule, Steven Sherman

Kama Biblia nyingine hazijatajwa, dondoo zote za kunukuu Biblia zinatumia Swahili Union Version (SUV): Haki miliki -1952, 1997: kwa: Chama cha Biblia cha Tanzania na Chama cha Biblia cha Kenya. Haki zote zimehifadhiwa.

GMI Publications ni idara ya Grace Ministries International; misheni ifanyayo kazi na dhehebu la Kanisa la Neema (Grace Church) duniani, pamoja na Wakristo wote wanaomwamini Yesu Kristo kuwa Mwokozi wao.

YALIYOMO

UTANGULIZI **1**

MWANDISHI **1**

KUSUDI LA KUANDIKWA KWA I YOHANA **4**

MAFUNDISHO MAKUU YA 1 YOHANA **7**

FUNDISHO #1 - KUONESHA WAZI USHIRIKA WETU 7
FUNDISHO #2 - KUONGEZA FURAHA 10
FUNDISHO #3 - KUZUIA DHAMBI 12
FUNDISHO #4 - KUWALINDA WATAKATIFU WA MUNGU 17
FUNDISHO #5 - KUTANGAZA MSAMAHA WA DHAMBI 20
FUNDISHO #6 - KUUENDELEZA UPENDO KATI YA WAKRISTO 24
FUNDISHO #7 - KUWAPA WAKRISTO UHAKIKA WA WOKOVU 30

MWISHO **35**

UTANGULIZI

Biblia ni Neno la Mungu. Mtume Paulo alilithibitisha wazo hilo katika 2 Timotheo 3:16. Mungu alisema na watu akiwapa makusudi yake katika vitabu 66. Kitabu cha kwanza kinaitwa Mwanzo na kiliandikwa na Musa miaka 1500 K.K. (Kabla ya Kristo kuzaliwa). Kitabu cha mwisho kiliandikwa na mtume Yohana miaka 95 B.K. (Baada ya kuzaliwa Kristo). Mtume Yohana alikuwa mtume wa mwisho na pia mwandishi wa mwisho wa Neno la Mungu, kwa maana aliishi mpaka akawa mzee sana. Kwa hakika aliishi miaka zaidi ya 60 baada ya kufa na kufufuka kwa Bwana Yesu. Kwa sababu hiyo tunaweza kujifunza katika vitabu vya Yohana hali ya Wakristo na namna walivyoishi na kufikiri katika miaka mingi ile baada ya Yesu kupaa kwenda mbinguni. Vilevile tunaweza kuitambua hali ya viongozi wa kanisa katika kipindi kile na mambo makubwa yaliyofanywa kati ya Wakristo na viongozi wao.

Ijapokuwa barua za Yohana hazitaji mahali Yohana alipokuwepo wakati alipoziandika, inaaminika kwamba mtume Yohana alikuwa katika mji wa Efeso katika jimbo la Asia Ndogo. Hapo ndipo Yohana alipoishi miaka yake ya mwisho duniani. Tarehe ya kuandikwa kwa waraka huu ni yapata 85-90 B.K.

Walioandikiwa waraka huu ni kundi la Wakristo au makundi ya Wakristo walioishi katika Asia Ndogo na ni wazi kwamba walimfahamu mtume Yohana vizuri. Soma 2:7, 18, 20, 21, 24, 27; 3:11 na utatambua kwamba waumini hawa walikuwa Wakristo wa siku nyingi. Habari hiyo inathibitishwa na hali ya kwamba tunajua walimu na wahubiri wengi walihudumu karibu na Efeso kwa miaka mingi kabla ya Yohana kuandika nyaraka zake. Kati yao ni Paulo (Mdo 18:14, 24-26), Trofimo (Mdo 21:29), jamii ya Onesiforo (2 Tim 1:16-18; 4:19) na Timotheo (1 Tim 1:3).

Inaonekana waliopokea waraka huu ni watu waliookoka kutoka katika upagani wa Mataifa. Kwanza, maandiko ya Agano la Kale hayatajwi katika barua hii. Kawaida waandishi wa Agano Jipya walinukuu Agano la Kale walipowaandikia Wayahudi na walipunguza maandiko kutoka Agano la Kale walipowaandikia watu wa Mataifa kwa kuwa Mataifa hawakulifahamu Agano la Kale. Pia katika 1 Yohana 5:21 kuna onyo juu ya kuabudu sanamu ambayo ilikuwa kawaida ya Mataifa na siyo Wayahudi katika kipindi hicho.

Yohana aliwajua wasomaji wa barua yake vizuri. Kwa sababu hii aliandika kwa upendo kwani aliwaita, *"Watoto wangu wapenzi."*

Kusudi la mafundisho yetu katika kitabu hiki ni kuyatambua mafundisho makuu ya waraka wa kwanza wa mtume Yohana na kuyatendea kazi katika maisha yetu. Tutapata msaada utakaotufaa sisi tunaoishi miaka mingi baada ya kuandikwa kwa kitabu hiki kwani kitabu chenyewe kiliandikwa kwa uongozi wa Roho Mtakatifu akiwa anatulenga hata sisi leo. Tuanze mafundisho yetu kwa kuangalia habari za mwandishi wa waraka huu.

MWANDISHI

MWANDISHI NI YOHANA

Maana ya jina "Yohana" ni "Yehova ni mwenye neema." Mara nyingi wazazi waliwapa watoto wao jina hilo kuonesha shukrani zao kwa Mungu kwa ajili ya kupewa zawadi ya mtoto (Tazama 1 Nya 3:15).

Mama yake Yohana aliitwa Salome (Mt 27:56; Mk 15:40; 16:1). Labda mama yake Yohana ndiye dada yake Maria, ambaye ni mama yake Yesu Kristo. Ikiwa ni hivi, ni kusema Yohana alikuwa ndugu wa Yesu (1Yn 19:25 na Mk 15:40). Baba wa Yohana alikuwa Zebedayo (Mt 4:21; Mk 1:19), mvuvi wa samaki katika Bahari ya Galilaya. Yohana alikuwa na ndugu aliyeitwa Yakobo (Mt 4:21), ndiye mtume aliyeuawa na Herode Agripa wa kwanza katika mwaka 44 B.K. (Mdo 12:1-2). Kwa kuisoma mistari ifuatayo, tunaona kwamba ndugu zake Yohana walikuwa matajiri.

- Marko 1:20 - Walikuwa na watumishi.
- Luka 8:3; Marko 15:40-41 - Salome alimsaidia Yesu Kristo alipoishi na kuhubiri hapa duniani.
- Marko 16:1 - Salome aliyaleta manukato kwa ajili ya kaburi la Yesu.
- Yohana 18:15-16 - Yohana alijuana na Kuhani Mkuu na aliweza kuingia katika behewa la nyumba yake wakati Yesu alipokamatwa. Kwa kawaida, makuhani wakubwa walikuwa watu wenye mali na waliheshimika.

Yohana alifundishwa na Yohana Mbatizaji (Yn 1:35), na vilevile alikuwa mwanafunzi wa Bwana Yesu. Yohana aliitwa kuwa "mvuvi wa watu" Mt 4:18-22; Mk 1:16-20; Lk 5:1-11). Kisha Yohana, pamoja na wengine kumi na mmoja, aliwekwa kuwa mtume (Mt 10:2-4; Mk 3:13-19; Lk 6:12-19).

a. Mambo gani matatu yanatajwa kuhusu "Kubarikiwa kwake" Yohana kama mwanafunzi wa Bwana Yesu katika Marko 3:14-15?

1 -

2 -

3 -

b. Alipomtumikia Bwana Yesu kabla Yesu hajafa, Yohana aliona na alijifunza mambo mengi katika maisha ya Yesu. Tazama sura na mistari iliyoorodheshwa hapo chini kuhusu mambo hayo. Soma kila andiko na uandike jambo moja Yohana alilojifunza pamoja na maana ya jambo hilo.

Marko 5:37 -

Luka 8:51 -

Mathayo 17:1; Marko 9:2 -

Luka 9:28 -

Marko 9:38 -

Luka 9:49 -

Luka 9:54 -

Marko 10:35 -

Marko 13:3 -

Luka 22:8 -

Yohana 13:23,25 -

Mathayo 26:37 -

Marko 14:33,37 -

Mathayo 26:56 -

Yohana 18:15-16 -

Yohana 19:26 -

Yohana 20:2-3 -

Yohana 1:1-7 -

Yohana 21:20-24 -

Kwa kusoma Wagalatia 2:9, tunaona kwamba Petro, Yakobo na Yohana walikuwa viongozi wa kanisa lililokuwa Yerusalemu kwa muda baada ya siku ya Pentekoste. Soma maandiko yanayofuata ili uone mambo aliyoyafanya Yohana katika muda huo: Matendo 3:1; 4:1-22; 8:14-15.

Yohana aliishi miaka yake ya mwisho katika mji wa Efeso. Efeso ilikuwa mji mkubwa katika Asia Ndogo na hapo ndipo mahali ambapo Yohana alifundisha, alihubiri, na aliandika (nyaraka au vitabu).

MWANDISHI YOHANA ALIMSHUHUDIA YESU KRISTO KWA MACHO YAKE MWENYEWE

Yohana anasema katika 1 Yohana 1:1 kwamba aliyoyahubiri juu ya Neno la Uzima ni yale aliyoyaona, aliyoyasikia na aliyoyagusa mwenyewe. Habari anayoitoa inahusu mambo yaliyofanyika katika "historia"; yaani Mungu wa milele alisikika akinena na alionekana akitenda. Yohana alikuwa akithibitisha habari aliyoihubiri kwa kusema kwamba, "Mimi mwenyewe nilikuwepo nikiona kwa macho yangu." Kwa sababu aliyaona mambo hayo yote mwenyewe, aliweza kuyahubiri kwa uhodari na mamlaka. Sharti moja la kuwa mtume wa Yesu Kristo lilikuwa uwezo wa mtu kusema amemwona Yesu kwa macho yake mwenyewe. Yohana anauthibitisha utume wake na mamlaka yake wakati anapodai amemwona Yesu na kwamba ametembea naye akisikiliza mafundisho yake.

MWANDISHI YOHANA ALIANDIKA KWA MAMLAKA KUTOKA KWA MWENYEZI MUNGU

Kwa sababu Yohana alijua kuwa mamlaka yake yametoka kwa Mwenyezi Mungu, hakusita kuwaita watu waongo, wadanganyifu, na wapinga Kristo. Alijihakikishia kuwa anao uwezo wa kumtambua mtu anayemjua Bwana Mungu na ambaye hamjui Bwana Mungu; aliye na Bwana Mungu na asiye na Bwana Mungu; aliye na uzima wa milele na asiye na uzima wa milele; anayetembea gizani au anayetembea nuruni; kama mtu ni mtoto wa Bwana Mungu au ni mtoto wa Shetani. Yohana alijua mamlaka yake hayajatokana na mitume wengine. Bali amri zote alizoziandika alizitambua kuwa ni za Mungu Mwenyezi (3:23, 24; 5:3), nyingine za Kristo (2:7; 2 Yn 5), na nyingine zake mwenyewe (2 Yn 10, 11; 3 Yn 9). Lakini hakutofautisha amri hizi, kwani zote ni za Mungu aliyemwongoza Yohana katika kuandika, na Wakristo wanapaswa kuzitii zote.

MWANDISHI YOHANA ALIANDIKA KAMA "MZEE" ANAYEHESHIMIWA

Yohana aliishi miaka mingi. Tuseme, kati ya mitume walioishi na Bwana Yesu hapa duniani, yeye alikuwa mzee kuliko wote. Neno "mzee" (2 na 3 Yn 1) linaonesha kukubaliwa kwake na linaonesha kwamba Yohana alikuwa na mamlaka ya kipekee katika makanisa ya wakati ule. Kama "mzee," uongozi wake ulikubaliwa na wote, na aliweza kuyaongoza makanisa ya Asia karibu na Efeso.

MWANDISHI YOHANA ALIANDIKA KAMA "KIONGOZI"

Kama mtu aliyeishi miaka mingi, Yohana alikuwa na sifa mbalimbali za uongozi. Neno moja kubwa la waraka wa kwanza wa Yohana ni "kujua." Kama mtu aliyewahi kumwona Bwana Yesu Kristo kwa macho yake mwenyewe, hali hiyo ilimpa Yohana maarifa mengi. Kiongozi anayefaa ni yule anayekubali kuwapa wengine maarifa aliyo nayo kama vile Yohana alivyofanya.

Pia Yohana alionesha “hekima” kwa namna alivyoitumia akili yake. Kuwa na akili ni kitu kimoja; kuitumia akili hiyo ipasvyo ni kitu kingine.

Vilevile Yohana ni mfano mzuri wa “kujitoa” kwa ajili ya umoja wa waumini. Katika barua zake anakazia sana habari ya ushirikiano na upendo.

Yohana aliwakumbusha waumini maneno haya: *“Wapenzi, sasa tu wana wa Mungu, wala haijadhihirika bado tutakavyokuwa; lakini twajua ya kuwa atakapodhihirishwa, tutafanana naye; kwa maana tutamwona kama alivyo.”* Paulo na Yohana hawakuogopa kufa kwa sababu walijua kwamba walipewa ahadi ya kumwona Bwana Yesu uso kwa uso tena. Walikumbuka tumaini hilo kila siku na lilizalisha tabia ya utakakifu katika maisha yao. Tabia hiyo iliwawezesha kuwa viongozi wazuri.

Bila kujisifu, Yohana hakuchoka kuwakumbusha wasomaji wake kwamba yeye alitembea na kusemezana na Yesu. Yesu mwenyewe alikuwa mfano wake wa kweli na Yohana alijifunza mengi kwa Bwana Yesu ambaye aliyabadilisha sana maisha ya mtume Yohana.

KUSUDI LA KUANDIKWA KWA I YOHANA

Waraka wa kwanza wa Yohana uliandikwa kwa makusudi mbalimbali. Kwa upande mmoja tunaweza kusema aliuandika kutokana na moyo wake wa kichungaji. Lakini kwa upande mwingine, tunaweza kusema kwamba Yohana aliuandika kutokana na moyo wake wa kuhoji na kuishindania imani. Tujifunze juu ya mambo hayo mawili.

YOHANA ALIKUSUDIA KUWACHUNGA KAMA MCHUNGAJI WAO

Katika kipindi kile Wakristo walikuwa wakivamiwa na hila na udanganyifu wa Shetani. Wakristo walikuwa wakipigana wao kwa wao na wengine walianza kuyapenda mambo maovu ya dunia. Wengine walipata mashaka juu ya wokovu wao na baadhi waliojiita “Wakristo” waliliacha Kanisa moja kwa moja (2:19).

Wale waliobaki walikuwa wakijiuliza: “Ni kwa namna gani tunaweza kujua kama sisi ni Wakristo kweli?” Hali hii ilisababisha Mtume Yohana awatie moyo kwa kuwafundisha kuwa wokovu walio nao ni wa milele. Yohana alitamani sana kuwaongoza waumini hawa kufikia ufahamu na imani itakayozaa matunda ya kikristo katika maisha yao. Yohana alilijibu swali lao kwa kutoa mambo makuu matatu yanayothibitisha wameokoka kweli na wana uhusiano na Mungu. Tazama mambo hayo matatu:

Uthibitisho wa kwanza ni maisha yao matakatifu

Yohana alitaka wasomaji wake waelewe uthibitisho mmojawapo wa kwamba wameokaoka kweli ni kuwa na mabadiliko katika mwenendo na silika zao. Kipimo cha utakatifu na haki ni utiifu. Yohana alitaka watambue jinsi ambavyo wamekuwa watiifu tofauti na maisha yao kabla hawajampokea Yesu. Si kusema Wakristo hawatendi dhambi yo yote, bali Wakristo ni watu wenye kukua na kuendelea katika haki. Kawaida ya Wakristo ni kubadilika taratibu kupitia maisha yao yote ili polepole maisha yao yaanze kufanana na mafundisho ya Neno la Mungu. Yohana anasema mabadiliko hayo yanayoonekana katika maisha yao ni uthibitisho wa kwamba wameokoka kweli.

Uthibitisho wa pili ni upendo wao

Uthibitisho wa pili wa wokovu wao ni ukweli wa muungano walio nao katikati yao kama Wakristo. Yohana anahoji Mungu ni upendo na upendo unatoka kwake. Hivyo Yohana anasema kila mtu anayesema anamjua Mungu, ni lazima awe na upendo kwa wengine. Vilevile anadai wanaoshindwa kuonesha upendo kwa wengine, wanajidanganya wenyewe. Anawasihi kuwa na upendo, lakini zaidi anauinua upendo huo kama uthibitisho wa kwamba wenyewe ni watoto wa Mungu aliye pendo.

Uthibitisho wa tatu ni yale wanayoamini kuhusu Yesu

Yohana anasema kwamba haiwezekani mtu kuwa Mkristo ikiwa mtu huyo hayaamini mambo fulani kuhusu Yesu Kristo. Mkristo ni mtu anayeamini kwamba Mwana wa Mungu, aliyekuwepo tangu milele, aliye nafsi ya pili katika utatu wa Mungu, alifanyika kuwa mwanadamu. Tuseme ni lazima mtu aamini kwamba Yesu Kristo alivaa mwili wa kibinadamu katika historia ya dunia, na alikufa kwa ajili dhambi za wanadamu, na mwishoni akafufuka kutoka wafu. Huu ndiyo msingi wa elimu inayomtambulisha mtu kuwa Mkristo wa kweli. Hoja ya Yohana ni kusema wakiamini habari hizo wajue wameokoka na wenyewe ni Wakristo hakika. Alitaka waifahamu imani yao kuwa ndiyo uthibitisho wa kwamba wao ni watoto wa Mungu kweli kweli.

Mathibitisho haya matatu yanatakiwa kuonekana katika maisha ya mtu ye yote anayesema “mimi ni Mkristo.” Sisi sote tunapaswa kujiangalia na kujichunguza ili kuhakikisha kama kweli sisi ni Wakristo. Tukiona mabadiliko ya utakatifu na haki katika maisha yetu, tukiona tunapendana, na tukiona tumeuamini ukweli wa Neno la Mungu kuhusu Kristo, tunaweza kutulia na kujua kwa uhakika sisi ni Wakristo waliookoka kweli. Katika hayo Yohana anawaandikia kama mchungaji anayejali sana maendeleo ya wasomaji wake katika Kristo.

YOHANA ALIKUSUDIA KUISHINDANIA IMANI DHIDI YA WALIMU WA UONGO

Vilevile Yohana aliandika kwa kusudi la kuishindania imani ya kweli. Hali katika Kanisa ilikuwa mbaya kwa sababu ya walimu wengine wa uongo ambao walikuwa wanafundisha mafundisho yao ya uongo katika makanisa (2:26; 3:7). Makanisa ya Asia yalikuwa katika hatari kwa sababu ya mafundisho ya kundi la watu walioitwa “watu wenye kufahamu”(Gnostics kwa Kiingereza). Mafundisho yao yalisimama kinyume na mafundisho ya mitume wa Kanisa.

Watu wengi walikuwa wakitafuta kupewa nuru lakini kwa hakika wengi walifikishwa katika kudanganywa na kupelekwa pembeni mwa ukweli ulio katika Kristo. Waliowadanganya watu hawa ni kundi lile la walimu, yaani, “watu wenye kufahamu” (gnostics). Watu wengine waliliacha Kanisa la kweli wakiunda kundi lao lililofundisha habari njema isiyopatana na ile iliyofundishwa na Yesu na mitume. Tendo hili la watu hao kuliacha Kanisa na kuyafuata mafundisho mengine, lilileta mashaka mioyoni mwa Wakristo waliobaki kanisani. Fujo na mashaka viliingia katika Kanisa hadi wengine wakaanza kuondoka na kusambaa. Yohana alikuwa akiandika kusudi awapatie Wakristo nguvu ya kusimama imara.

Walimu hawa wa uongo walijulikana kwa namna tatu. Sifa hizo tatu zinaonesha mafundisho yao kuwa uongo na nia yao kuwa mbaya wakitaka kuvuta watu pembeni. Kwanza, Yohana anawaita “manabii wa uongo” (4:1). Nabii ni mwalimu anayesema akiongozwa na uwezo usio wake yeye mwenyewe. Nabii wa kweli ni kinywa cha Roho Mtakatifu lakini nabii wa uongo ni kinywa cha roho ya uovu. Pili, Yohana anasema walimu hawa wa uongo ni “wadanganyifu” (2 Yn 1:7). Jina hili linaonesha kwamba watu hawa ni wenye kuwaongoza wengine pembeni ili wapotee. Tatu, Yohana aliwatambulisha kuwa “wapinga Kristo” (2:26; 4:2; 2 Yn 7) kwa sababu msingi wa mafundisho yao ni kukana uungu na ubinadamu wa Yesu Kristo. Kwanza watu hawa walikubaliwa kuwa watu wa Kanisa lakini baadaye waliacha Kanisa (2:19) na walienda duniani kuutangaza uongo na maovu yao (4:1; 2 Yn 7).

Kosa la walimu hawa wa uongo lilikuwa katika elimu na teolojia yao (2:26; 4:2; 2 Yn. 7), na hata katika maana ya maisha matakatifu (3:7). Kosa lao moja la elimu lilikuwa juu ya ubinadamu wa Yesu. Walisema kwamba Yesu ni Kristo (2:22). Hawakukana kwamba Yesu alikuwa Masihi lakini waliukana ubinadamu wake. Mafundisho haya ya uongo yalikana kwamba “Yesu Kristo amekuja katika mwili” (4:2; 2 Yn. 7). Pia hawakumkubali Yesu Kristo kuwa njia pekee ya kumfikia Mungu. Hivi waliamini kwamba wataweza kumfikia au kumkaribia Mungu kwa njia ya akili zao wenyewe. Walisema kwamba imani haina maana katika wokovu, na vilevile matendo yanayofanyika katika maisha ya muumini hayana maana katika wokovu.

Kwa kuipinga elimu hii ya uongo, Yohana anauthibitisha ukweli wa ubinadamu wa Yesu Kristo; yaani kuja kwake duniani na kuzaliwa kama mtu. Yohana anakaza kwamba Yesu alikuwepo tangu mwanzo, na hapa duniani katika maisha ya Yohana Yesu alisikika kwa masikio ya watu na alionekana kwa macho yao, na aliguswa kwa kwa mikono ya mashahidi wengi (1:1-3; 4:14). Yeye aliyekuwepo tangu mwanzo ndiye yeye ambaye mitume walimsikia, walimwona na kumgusa. Haiwezekani kutofautisha Yesu Kristo, yeye aliyezaliwa na yeye aliyekuwepo tangu milele. Kristo na Yesu ni mmoja, Yesu ni Mungu na Yesu ni mwanadamu wakati mmoja.

Maana ya maisha matakatifu ilifundishwa kimakosa na walimu wa uongo wakimaanisha kwamba kutenda dhambi kwa Mkristo hakuna madhara. Vilevile walifundisha kwamba dhambi haiwezi kuzuia ushirika wetu na Mungu. Yohana anasema waziwazi kwamba hao wanaofundisha elimu hiyo ni waongo au wanajidanganya wenyewe au wanamfanya Mungu kuwa mwongo (1:6, 8, 10). Mungu amejifunua kuwa ni mwenye haki, na kwa sababu hii haiwezekani kushirikiana naye bila kuwa mtakatifu na mwenye haki (2:4, 6).

a. Basi, unaona nini kati ya amri za Mungu na maisha ya Mkristo (2:9; 4:20)?

Walimu wa uongo walisema kwamba “wanamjua Mungu,” “wanakaa ndani ya Mungu,” na “wanaishi katika nuru.” Lakini waliishi bila haki na upendo. Watu hawa ni “waongo.” Hawawezi kusema kwamba wao ni wenye haki kama hawatendi haki (2:25-3:10). Yohana anasema kwamba “Mungu ni nuru” na “Mungu ni upendo.” Kwa sababu hii, giza la dhambi na machukizo ni matendo yasiyopatana na mtu anayemjua Mungu. Tunaweza kufahamu kwamba tunamjua Mungu kwa kuzitii amri zake, kwa mfano kuwapenda ndugu zetu (2:3; 3:14).

MAKUSUDI YA YOHANA KUIANDIKA BARUA YAKE

Tumeona kwamba kusudi la Yohana kuandika barua hii lilikuwa kujenga mawazo ya Wakristo na kukanusha mafundisho ya walimu wa uongo. Soma mistari hii na andika maneno yale yanayotuambia makusudi yake hasa ya kuandika barua hii; yaani makusudi ambayo Yohana mwenyewe anayataja.

1:3 -

1:4 -

2:1 -

2:7-8 -

2:26 -

5:13 -

MAFUNDISHO MAKUU YA 1 YOHANA

Umeshaangalia mistari saba katika 1 Yohana yanayoeleza sababu za Yohana kuiandika barua hii. Sasa tuchunguze kwa ndani zaidi makusudi hayo saba kwa kuwa makusudi hayo ni mafundisho makuu ya 1 Yohana. Kusudi la kwanza ni:

FUNDISHO #1 - KUONESHA WAZI USHIRIKA WETU

Kusudi la kwanza la barua hii ya 1 Yohana ni kwa wasomaji wapate kuufurahia ushirika wa kweli wa Kikristo. Ushirika huo wa kweli ni ule ambao Bwana Yesu alikuwa nao na wanafunzi wake alipokuwa hapa duniani. Lakini ushirika huo si kwa ajili ya wanafunzi wale kumi na wawili tu. Bali ushirika huo uliendelezwa na Roho Mtakatifu wakati amekuja kukaa ndani ya waumini. Ushirika huo ni kwa vizazi vyote, yaani ni kwa Wakristo wote, hata leo, kwa sababu, *"Ushirika wetu ni pamoja na Baba na Mwana wake Yesu Kristo"* (1:3). Yohana alitaka mambo aliyoyasikia na kuyaona wakati alipohusiana na Kristo, kuwa kawaida katika maisha ya Wakristo wote. Kusudi la Yohana la kutangaza Habari Njema katika 1 Yohana halikuwa kuwashuhudia watu ili waokoke (kwa sababu wasomaji wake walikuwa wameshaokoka - 2:27), bali alitaka wapate kuujua na kuutendea kazi ushirika waliokuwa nao katika Kristo.

Neno "ushirika/kushirikiana" linatajwa mara 4 katika sura ya kwanza ya barua hii. Maana ya neno hili ni muungano na mapatano. Katika Agano Jipya ushirika ni neno linaloonesha muungano wa ndani ulio kati ya waumini na Mungu na kati ya waumini na waumini. Msingi wa ushirika huo ni muungano wetu katika Kristo. Hali hii ya kuwa katika Kristo inapatikana kwa kazi ya Roho Mtakatifu wakati anapotubatiza katika Kristo (1 Kor 12:13), tendo linalotuunga pamoja na Kristo na pamoja na waumini wenzetu wote (yaani, tunakuwa mtu mmoja katika Kristo).

Muungano huo unatambulika:

- Wakati Wakristo wanasaidiana kwa kuzitoa nguvu zao au mali zao ili kuyatimiza mahitaji ya wengine (Rum 15:26; 2 Kor 9:13; Ebr 13:16; 2 Kor. 8:4).
- Katika muungano wa kiroho kati ya waumini na Mungu na waumini kwa waumini (1 Kor 1:9; 2 Kor 13:14; Gal 2:9; Flp 2:1; 1 Yn 1:3,6,7).
- Katika kuungana pamoja wakifanya kazi ya kueneza Habari Njema, au kuungana katika mateso na mambo mengine (Mdo 2:42; 1 Kor 10:16; 2 Kor 6:4; Flp 1:5; 3:10; Flm 6).

Ushirika wa Kikristo una sehemu mbili. Sehemu ya kwanza inaoneshwa na mfano wa mstari uliochorwa ukisimama wima (vertical) na ya pili inaoneshwa na mfano wa mstari uliolala (horizontal). Ushirika wa wima (vertical) ni ule unaoelezwa na Yohana alipoandika: *"Na ushirika wetu ni pamoja na Baba na Mwana wake Yesu Kristo"* (1:3), yaani uhusiano wetu na Mungu. Sehemu ya pili ya ushirika wa Kikristo inaonesha na mstari wa kulala, yaani ni uhusiano kati ya waumini.



a. Tunafundishwa nini juu ya Baba na Mwana wake katika 1 Yohana 1:1-3? (Soma Injili ya Yohana 1:1-18 na 20:30-31).

b. Mafundisho haya yana maana gani katika maisha yetu ya Kikristo?

Hakuna mtu anayeweza kuufurahia ushirika huo kama yeye bado hajawa mtoto wa Mungu (1 Yn 1:12). Tunafanywa kuwa wana wa Mungu kwa kumpokea Bwana Yesu kuwa Mwokozi wetu. Haiwezekani kuwa na ushirika na Mungu Baba bila kumjua na kumwamini Mwana wake Yesu Kristo (Yn 2:22-24; 4:2, 3, 15; 5:1, 7, 10-12, 20). Katika maandiko haya Yohana anaongea uhusiano wetu na Mungu Baba na uhusiano wetu na Yesu Kristo bila kutaja ushirika wetu pamoja na Roho Mtakatifu. Lakini tunafundishwa kuhusu sehemu hii ya ushirika wetu katika barua za Mtume Paulo (2 Kor 13:14; Flp 2:1).

c. Soma maandiko haya matatu na jibu maswali yafuatayo:

1:5-7 - Mungu ni nini? Maana yake nini? -

1:8-10 - Sisi ni wenye kufanya nini? -

2:1-2 - Sisi tunaye nani? Katika nafasi hiyo anatufanyia nini? -

d. Kuna masharti gani kwa yule anayetaka kushirikiana na Mungu katika mistari hii miwili?

1:7 –

1:9 –

e. Andika maelezo yote ya maisha ya Kikristo yanayotajwa katika mistari ya 1:5-2:2. Chunguza namna maisha ya Kikristo yanavyoelezwa waziwazi.

Ushirikiano kati ya Mkristo na Mungu ni msingi wa ushirikiano ulio kati ya Wakristo. Ushirika wa Kikristo si wima tu; yaani si kati ya Wakristo na Mungu tu, bali ni mahusiano yale yaliyo kati yetu kama Wakristo vilevile. Ushirikiano huo, ulio kati ya Wakristo, ndio unaoleta matunda mazuri katika maisha ya Wakristo.

Ushirikiano huo unaonekana kwanza katika matendo ya Wakristo katika kusaidiana (Rum 15:26; Mdo 4:35; 2 Kor 9:13; Ebr 13:16). Unafanana na jinsi Bwana Yesu alivyoigawa mikate mitano na samaki wawili wakishirikiana wote katika chakula (1 Yn 6:11). Paulo anawahimiza Wakristo kuwa na ushirikiano huo akisema, *"Kwa mahitaji ya watakatifu, mkifuata ukarimu; katika kukaribisha wageni, mkijitahidi"* (Rum 12:13).

Vilevile, ushirikiano wa Kikristo unaonekana katika shughuli za Wakristo pale wanapojengana katika maisha yao ya kiroho. Yaani, ni njia ya Mkristo kumsaidia mwenzake amfahamu Mungu na abadilike katika maisha yake ya kiroho. Kwa jinsi hii ushirikiano ulio kati ya

Wakristo unafanya kila Mkristo awe na uhusiano bora na Mungu. Ushirikiano huo unaonekana katika maneno kama kufundishana, kujengana, kuonyana, kusameheana, n.k. Katika ushirika huo Wakristo wote wanapokea na wanatoa wakitendeana mema. Mtume Paulo alitoa mfano juu ya habari hii wakati alipowaambia Warumi: *"Kwa maana ninatamani sana kuwaona, nipate kuwapa karama ya rohoni, ili mfanywe imara; yaani tufarijiane mimi na ninyi, kila mtu kwa imani ya mwenzake, yenu na yangu"* (Rum 1:11-12).

Misingi muhimu ya ushirikiano wa Kikristo ni upendo na unyenyekevu. Upendo unamsukuma Mkristo kumtendea mwenzake kwa wema na unyeyekevu unamfanya amjali mwenzake akihesabu mahitaji ya mwenzake kuwa muhimu kuliko mahitaji yake binafsi. Katika kupendana na kunyenyekeana wote wanafaidika kwa kuwa mmoja anamsaidia mwenzake na mwenyewe anasaidiwa, wakitenda mema na kutendewa mema.

Kwa kifupi tazama mambo mbalimbali yahusuyo ushirika:

- Ushirika wa tabia ya Uungu - 2 Pet 1:4
- Ushirika wa Roho – Flp 2:1
- Ushirika wa watakatifu - 1 Yoh 1:3
- Ushirika wa vitu - Rum 12:13
- Ushirika wa Mateso ya Kikristo - Fil 3:10; Kol 1:24; 2 Tim 1:8; 1 Pet 4:13
- Ushirika wa utukufu na umiliki wa Kikristo - 2 Tim 2:12; 1 Pet 5:1

<u>Maana Kwetu Leo</u>

1. Msingi wa ushirika wetu ni nini? (Rum 12:5; 1 Yn 1:3)

2. Kwa nini Wakristo leo wanahitaji ushirika?

3. Mambo gani yanazuia ushirika?

Ebr 5:11-12 -

Rum 12:1-2 -

Ebr 12:5 -

1 Kor 12 -

4. Biblia inatufundisha kwamba ushirika wa kweli una mambo yanayoonekana wazi-wazi katika maisha ya Wakristo. Basi, kanisa lisiloonesha tabia hizi lina ugonjwa. Soma kila andiko linalofuata na andika maneno makubwa juu ya ushirika.

Mdo 2:42 -

Mdo 2:44 -

Mdo 2:45 -

Mdo 2:46 -

Mdo 2:47 -

Yoh 15:17; 1 Yoh 3:23 -

Rum 15:7 -

Rum 15:14; Kol 3:16 -

1 Kor 12:26 -

Efe 4:32 -

Efe 5:21 -

Yak 5:16 -

1 Yoh 1:7 -

Efe 4:31-32; Kol 3:12-13; Rum 14:1 -

Kol 3:16 -

1 Thes 5:11; Ebr 3:12-13 -

Efe 5:18-20 -

Gal 5:13-14 -

Gal 6:2 -

1 Pet 4:7-10 -

5. Eleza jinsi kanisa lako linavyofaulu katika ushirikiano wa kibiblia.

6. Eleza jinsi kanisa lako linavyofeli katika ushirikiano wa kibiblia.

Mstari Mkuu

1 Yohana 1:7 – "Bali tukienenda katika nuru, kama yeye alivyo katika nuru, tunashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote."

FUNDISHO #2 - KUONGEZA FURAHA

Kusudi la pili la kuandika barua hii ni kuonesha jinsi Wakristo walivyo na nafasi pekee ya kuwa na furaha inayoongezeka katika maisha yao ya Kikristo. Yohana anatumia neno "furaha" mara moja tu katika barua hii lakini wazo la furaha linaonekana katika sehemu zote za waraka wake. Kwa Yohana, furaha ni hali inayopatikana katika ushirikiano na Mungu. Yohana huonesha haiwezekani kuwa na furaha ya kweli bila kushirikiana na Mungu na watoto wake. Yeye anasisitiza kuwa yule atakayeendeleza ushirikiano wake na Mungu atakuwa mtu wa furaha. Pia, wazo la kujazwa furaha linaonekana katika maandiko mengine ya Yohana (k.m. Yn 3:29; 15:11; 16:24; 17:13; 2 Yn 12). Kwa Yohana furaha daima inapatikana katika ushirikiano na Mungu na pia katika ushirikiano pamoja na watu wa Mungu.

Kwa sababu ya dhambi, tunajua haiwezekani kuwa na furaha kamili katika dunia hii. Dhambi ni msingi wa masikitiko na ukosefu wa furaha. Dhambi inaahidi furaha, lakini kwa hakika inaleta masikitiko tu. Anasa na furaha ya dhambi inadumu kwa muda mfupi tu (Ebr 11:25) wakati raha ya Mungu inaendelea milele (Zab 16:11). Kwa sababu hii 1 Yohana 1:4 haiongei furaha yetu hapa duniani tu lakini vilevile furaha yetu ya milele mbinguni.

Mifano miwili ya furaha hapa duniani inaonekana katika maisha ya mtume Paulo. Paulo aliwafurahia wale waliompokea Bwana Yesu katika miji ya Wafilipi na Thesalonike (Flp 4:1; 1 Thes 2:19-20).

Mungu anataka watu wake wawe na furaha mioyoni mwao. Yesu alionesha nia hiyo katika mafundisho yake. Aliwashawishi watu kutii na kutendea kazi mafundisho yake akiwa na kusudi la kuifanikisha furaha yao (Yn 15:11). Wakati alipokuwa akiwaombea kwa Mungu alionesha tena furaha yao ni sehemu ya mapenzi yake (Yn 17:13).

Daima katika Neno la Mungu furaha ya kweli huelezwa kupatikana katika Mungu na mambo yake. Kwa mfano, shina au msingi pekee wa furaha ni Bwana mwenyewe (Isa 29:19; Hab 3:17-18), Wakristo wanaweza kuwa na furaha kwa sababu ya uwezo wa Mungu (Mdo 8:5-8); uwepo wa Kristo huleta furaha (Yn 16:22; 20:20); kuna furaha katika kutazamia thawabu (Mt 5:12; Lk 6:23); kuna furaha katika Habari Njema kuhubiriwa (Flp 1:18); maombi ni jambo linaloleta furaha (Yn 16:24); na hata maendeleo mazuri ya waumini wenzetu hutupa furaha (Rum 12:15; 2 Kor 7:13,16; 3 Yn 2-4).

a. Katika waraka wake Yohana anaeleza ni mambo gani yanayoongeza furaha yetu?

1:3,6,7 -

1:6,8,10 -

5:13 -

1:9 -

Tuchunguze zaidi 1 Yohana 1:4, *"Na haya tunayaandika, ili furaha yetu itimizwe."* Neno *"haya"* linahusu barua nzima iliyoandikwa kwa waumini kusudi furaha yao ikamilishwe. *"Furaha"* inayotajwa hapa ni furaha tele ya Wakristo ya wakati wote na katika hali zote (soma Mdo 5:41; 2 Kor 8:2). Yesu Kristo mwenyewe, anayeishi ndani ya kila Mkristo, ni mfano kamili wa vile tunavyoweza kuwa na furaha ijapokuwa magumu ya kila namna yanatupata. *"Tukimtazama Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu; ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu, naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu"* (Ebr 12:2). Furaha yake Yesu ilikuwa kuyafanya mapenzi ya Baba yake na kuungojea utukufu utakaofuata. Habari hii ni mfano kwetu wenye kututia moyo.

Yesu aliwaambia wanafunzi wake, *"Hayo nimewaambia, ili furaha yangu iwe ndani yenu, na furaha yenu itimizwe"* (Yn 15:11). Maana ya *"hayo"* ni nini? Tazama mstari wa kumi. *"Mkizishika amri zangu, mtakaa katika pendo langu; kama vile mimi nilivyozishika amri za Baba yangu na kukaa katika pendo lake."* Kanuni tunayotaka kuikaza hapa ni hii: Msingi wa furaha iliyo tele, inayoendelea milele, ni kujitoa katika kuyatii mapenzi ya Mungu kama yanavyoelezwa katika Neno lake. Maandiko yanayotangulia na yanayofuata mistari hii yanaonesha waziwazi namna tunavyoweza kuwa na furaha yake wakati wote na katika hali zote. Ni kwa "muungano" wetu na "ushirika" wetu pamoja na Kristo (Yn 15:4,5,7).

"Hayo", yaliyosemwa na Bwana Yesu katika Yohana 15:11, ni hali ile ya kumtii Yesu na kukaa ndani yake. Matokeo yake ni furaha. Katika 1 Yohana 1:4 *"haya"* yanaongea ushirika, na matokeo yake, vilevile, ni furaha. Dini ya Kikristo ni dini ya furaha kwa sababu ina ushirikiano pamoja na Kristo, ambaye ndani yake kuna furaha tele (Zab 16:11). Msingi wa furaha yote ni kazi ya Kristo msalabani, hivyo wokovu na furaha vinaunganishwa pamoja (Lk 2:10; Mdo 8:39; 16:34; 8:8).

<u>Maana kwetu leo</u>

1. Ni mambo gani yanayoharibu furaha katika maisha ya Mkristo?

Flp 4:1-4 -

Zab 51:1-12 -

2. Katika Zaburi 51, Daudi alifanya nini (alichukua hatua gani) kurudisha ushirika wake na Mungu?

Mst. 2 -

Mst. 7 -

Mst.12 -

3. Wakati tunapotenda dhambi, furaha yetu inapungua. Eleza jinsi furaha yetu inavyoweza kurudishwa katika 1 Yn 1:9; 2:12.

4. Wagalatia 5:22-23 inasema nini juu ya furaha?

5. Maana ya kuwa na furaha ya Bwana ni nini?

6. Ukichunguza maisha yako, je, unayo furaha ya Bwana katika maisha yako? Mambo gani yanapunguza furaha yako? Unaweza kufanya nini kuiongeza furaha yako kutokana na somo hilo?

Mstari Mkuu

1 Yohana 1:4 - "Na haya tunayaandika, ili furaha yetu itimizwe." (Tazama pia Yn 15:11; Rum 15:13)

FUNDISHO #3 - KUZUIA DHAMBI

Kusudi la tatu la kuandikwa kwa Waraka wa kwanza ya Yohana ni kuizuia dhambi katika maisha ya Mkristo. Habari ya dhambi inatajwa mara 27 katika barua hii. Yohana anatoa mafundisho mengi juu ya jambo hilo kwa sababu dhambi inaharibu ushirikiano wetu na Mungu na hivyo inapunguza furaha yetu kwa kuwa furaha ni tunda la ushirika wetu naye. Ikiwa tunakosa furaha katika maisha yetu ya Kikristo, labda ni kwa sababu kuna dhambi inayozuia ushirikiano wetu na Mungu. Kwa sababu hii ni lazima tuyafahamu ujumbe wa Yohana kuhusu dhambi unaoeleza jinsi tunavyoweza kuishinda.

Yohana anafundisha kila Mkristo anayo asili ya dhambi

Kanuni ya dhambi inaonekana katika maneno haya ya Yohana: *"Tukisema kwamba hatuna dhambi, tunajidanganya wenyewe, wala kweli haimo ndani yetu"* (1 Yn 1:8). Katika andiko hilo, sawasawa na Yohana 1:29, *"dhambi ya ulimwengu"* si matendo ya dhambi bali ni kanuni ya dhambi inayotawala ndani ya watu, hata Wakristo. Katika Yohana 1:8 dhambi inayoongelewa ni dhambi ya asili – hali ile ya dhambi tuliyorithi kutoka kwa Adamu ali-yeitenda dhambi ya kwanza. Ni hali ile ya dhambi ni kanuni ya dhambi kwa watu wote. Matendo ya dhambi yanatendeka kwa sababu ya tabia au asili ya dhambi iliyo katika kila mtu. Dhambi iliingia ulimwenguni kwa njia ya *"mtu mmoja"* (Rum 5:12), *"kwa kukosa mtu*

mmoja" (Rum 5:17), na kwa sababu ya *"kuasi kwake mtu mmoja"* (Rum 5:19). Mtu huyo ni Adamu, hivyo watu wote wamerithi asili yake ya dhambi na kwa sababu hiyo wanatenda matendo ya dhambi. Tukisema hatuna dhambi tunasema uongo na tunamfanya Mungu kuwa mwongo kwa kuwa watu wote wanayo asili ya dhambi. Kuna mtu mmoja tu asiye na asili ya dhambi na asiyetenda dhambi, ni Bwana Yesu Kristo, ambaye imeandikwa juu yake kwamba, *"Dhambi haimo ndani yake"* (1 Yn 3:5).

a. Soma maandiko haya na andika maneno mbalimbali ambayo Yohana anayatumia kwa ajili ya kuielezea dhambi.

1:6 -

1:9 -

2:16 -

3:4 -

3:12 –

5:17 -

b. Soma maandiko haya na andika matendo ya dhambi.

1:6; 2:4,22 -

2:9,11; 3:10 -

2:15 -

4:18 -

5:21 -

Dhambi ni kutomtii Mungu na tendo lo lote lisilo la haki

Yohana anaelezea dhambi kwa njia mbili katika barua yake. Kwanza, anasema dhambi ni kukataa kuitii sheria ya Mungu. Ndiyo maana alisema "*dhambi ni uasi"* (3:4). Neno *"uasi"* unahusu hali ya kuvunja sheria au kanuni (Yak 2:10). Wakati tunapoivunja sheria na maagizo ya Mungu tunamkosea Mungu, tunawakosea wengine na tunajikosea sisi wenyewe. Katika maelezo haya kipimo ni sheria na maagizo ya Mungu.

Maana ya pili ya dhambi ni *"kila lisilo la haki"* (5:17). Kila tendo lisilopatana na haki ya Mungu ni dhambi. Katika maelezo haya haki ni kipimo cha kuyapima matendo yetu kujua kama ni matendo ya dhambi au la. Tujue dhambi ni kuyaasi mapenzi ya Mungu na kuzivunja sheria zake takatifu na pia ni matendo yo yote yasiyoendana na haki ya Mungu Mtakatifu.

Ili tuweze kuishi maisha matakatifu ni muhimu tufahamu dhambi ilivyo katika asili yetu na pia katika matendo yetu. Yaani, ni lazima tutambue ubaya na uovu wa dhambi ili tuichukie. Tusiendelee kufikiri kuna dhambi yo yote isiyo na madhara makubwa. Dhambi zote ni mbaya na zote zinaleta uharibifu mkubwa.

Wakristo wanaagizwa kutotenda dhambi na wanaweza

Tumeshaona kuna asili ya dhambi ndani ya muumini inayomwongoza kutenda dhambi. Ijapokuwa ana asili hiyo ya dhambi anaambiwa na Mungu asitende dhambi. Kwa sababu Mkristo ana asili ya dhambi, Mkristo ana uwezo wa kutenda dhambi, lakini kwa sababu Yesu ameshinda na kuzivunja nguvu za dhambi msalabani, Mkristo anao uwezo vilevile wa kutotenda dhambi. Ingawa Mkristo anaweza kuanguka mara kwa mara katika dhambi ha-

paswi kuendelea katika dhambi kama kawaida ya maisha yake. Bali kila Mkristo ana uwezo wa kujiepusha na dhambi na hilo ndilo agizo na ni mapenzi ya Mungu.

1 Yohana 2:1 inatusihi hivi, *"Watoto wangu wadogo, nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi."* Hili ni kusudi kamili la Mungu. Kusudi hilo linakanusha wazo lile la walimu wa uongo waliosema kwamba dhambi ni lazima katika maisha ya mtoto wa Mungu. Yohana anaonesha waziwazi kwamba maisha yaliyo ya kweli, yaliyojaa furaha na yanayokua katika neema ya Mungu, ni maisha yanayochukia dhambi. Kama Wakristo tunaweza kuishinda dhambi na kuwa washindi kwa njia ya msaada ulio katika Bwana wetu Yesu Kristo.

Kwa Yohana kutotenda dhambi humaanisha hali endelevu

Tunasoma hivi katika I Yohana 3:6, *"Kila akaaye ndani yake hatendi dhambi; kila atendaye dhambi hakumwona yeye, wala hakumtambua."* Katika sarufi ya Kiyunani maneno "kukaa" na "kutenda" yanaongelea matendo yanayoendelea katika muda uliopo. Kila mtu anayeendelea kukaa ndani yake Kristo hawezi kukaa au kuendelea katika dhambi. Mstari huu hausemi kwamba Mkristo hawezi kufanya dhambi, lakini unasema kwamba Mkristo hawezi kuendelea katika kutenda dhambi kama kielelezo kikuu cha maisha yake. Yohana anakubali kwamba Wakristo wana asili ya dhambi na pia wanatenda dhambi mara kwa mara. Ndiyo sababu anaeleza jinsi wanavyopaswa kuungama dhambi zao mara moja na kutoendelea katika dhambi hizo (1:9). Lakini fundisho la mstari huu linahusu tabia za mtu au kawaida ya maisha yake. Kuendelea kukaa (kuishi) ndani ya Kristo na kuendelea kukaa (kuishi) ndani ya dhambi ni mambo mawili yasiyopatana na yasiyowezekana. Katika fundisho la Yohana, mtu anayeishi katika dhambi kama kawaida ya maisha yake ni mtu asiyemjua Kristo (Mt 7:21-23) na mtu anayemjua Kristo ana uwezo wa kukosea na kuanguka katika dhambi lakini wazo kuu la maisha yake ni lile la mtu mtiifu na siyo mwasi au mtenda dhambi.

Tabia mpya ya uungu huwasaidia Wakristo wasitende dhambi

Tunasoma katika 1 Yohana 3:9: *"Kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, kwa sababu uzao wake wakaa ndani yake; wala hawezi kutenda dhambi kwa sababu amezaliwa kutokana na Mungu."* Wale waliozaliwa na Mungu hawaendelei kufanya dhambi. Kila aliyezaliwa na Mungu, amepewa tabia ya Mungu ndani yake kama uzao wake (2 Pet 1:4; 1 Yn 3:9). Tabia hiyo ya uungu inatufanya tufanane na Bwana Yesu Kristo. Lakini kuna tofauti kubwa kati ya Bwana Yesu na sisi tuliozaliwa na Mungu leo. Tofauti hiyo ni kwamba Bwana Yesu alizaliwa na bikira Mariamu na kwa sababu hiyo hakurithi asili ya dhambi kama sisi tulivyoirithi wakati tulipozaliwa. Bwana Yesu hakuwa na asili ya dhambi na pia hakutenda dhambi. Hakika yeye hakuweza kufanya dhambi kwa kuwa yeye ni Mungu. Walakini, sisi tumezaliwa na asili ya dhambi na asili ile ingali imo ndani yetu ijapokuwa tumepewa tabia mpya ya uungu. Wakati sisi kama Wakristo tunapofanya dhambi, ni kwa sababu asili ya dhambi imeshinda katika kutuongoza au kutusukuma. Lakini tabia ile yetu mpya iliyo ndani ya kila Mkristo haikubali kutenda dhambi na kwa sababu hii kuna vita ndani yetu kati ya asili ya zamani na tabia mpya ya uungu. Katika maisha ya Mkristo, tabia ile ya uungu, kwa ujumla, inashinda asili ile ya dhambi katika vita hivyo. Tunasema "kwa ujumla" tukimaanisha kwamba mara kwa mara asili ya dhambi inaonja ushindi tunapoanguka katika dhambi, lakini zaidi tabia yetu mpya inapata ushindi. Mwisho wake maisha yetu yanaelezwa kuwa ya utiifu na siyo ya kuwa watenda dhambi.

Kujilinda kwa Wakristo huwasaidia kutotenda dhambi

1 Yohana 5:18 inasema hivi, *"Twajua ya kuwa kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi; bali yeye aliyezaliwa na Mungu hujilinda, wala yule mwovu hamgusi."* Mkristo anaweza kufanya dhambi mara moja moja lakini hawezi kutenda dhambi katika hali ya kuendelea ndani yake. Kwa nini? Kwanza, kwa sababu amezaliwa na Mungu. Pili, kwa sababu anajilinda kwa uwezo wa Mungu kusudi asili ya dhambi ipate kushindwa (Mt 26:41; Gal 5:16-17). Mkristo wa kweli atajikaza sana kuzuia dhambi katika maisha yake. Kwa mafun-

disho zaidi kuhusu wajibu wa Mkristo katika kuachana na dhambi soma Warumi 6:1-23 na 8:1-17).

Msingi wa ushindi wa Wakristo juu ya dhambi ni katika kazi ya Kristo msalabani

Msingi wa kushinda dhambi umewekwa wazi katika 1 Yohana 2:1-2, *"Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki, naye ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu, bali na kwa dhambi za ulimwengu wote."* Kama Wakristo tunapaswa kuelewa shida ya dhambi kati ya Mungu na kila anayemwamini Yesu imekwisha suluhishwa. Wakati mtu anapomkubali Kristo kuwa Mwokozi wake, Mungu anamsamehe dhambi zake zote kwa njia ya damu ya Yesu Kristo. "Dhambi zote" ina maana zote alizotenda tayari kabla hajaokoka, zote anazotenda katika muda uliopo, na zote ambazo atazitenda baadaye katika maisha yake ya Kikristo. Kwa sababu hii Mungu anamkubali muumini kuwa mwenye haki katika Kristo mara moja na kwa milele kwa kuwa amevalishwa haki ya Kristo.

Hivyo, Wakristo wanapotenda dhambi mara kwa mara haimaanishi hawakuwa Wakristo na pia haimaanishi wamepoteza ukristo au wokovu wao. Bali, baada ya kumpokea Bwana Yesu, dhambi zao huvunja ushirikiano nao na Mungu Baba na uhusiano ule unahitaji kutengenezwa ili uwe wa karibu tena. Sasa, wakati Wakristo wanapofanya dhambi, wana *"Mwombezi"* anayewasiliana na Mungu Baba juu ya dhambi hiyo. Mwombezi wao, Yesu Kristo aliye mbinguni, anawatetea. Si kusema Yesu anamwomba Mungu awahurumie na kusahau dhambi walizozifanya, Hapana! Bali anawatetea kwa sababu yeye (Bwana Yesu) ni *"mwenye haki"* na ametimiza matakwa yote ya sheria wakati alipojitoa msalabani kwa ajili yetu sisi wenye dhambi. Huu ni msingi wa Kristo kutuombea mbele ya Mungu anayekubali kazi ya Kristo kutufanya kuwa wenye haki (1 Pet 3:18).

Katika 1 Yohana 2:2, Yesu ni, *"kipatanisho kwa dhambi zetu."* Maana yake ni kumpitia Kristo Mungu *"anatusafisha"* na *"anatusamehe"* (1:7,9). Katika kufa kwake, Bwana Yesu alifanya upatanisho uliompendeza Mungu akilipa deni letu la dhambi. Bwana Yesu alifungua njia – yaani aliondoa kizuizi - kusudi watu wamfikie Mungu. Kilichofunga njia ni dhambi.

Katika Daraka la Sheria kondoo dume aliletwa kuwa sadaka ya dhambi kwa kufanya upatanisho (Hes 5:8). Lakini msalabani Kristo mwenyewe alikuwa sadaka ya upatanisho. Ni yeye aliyekuwa *"Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu"* (Yn 1:29). *"Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake"* (2 Kor 5:19). Hivi waumini ni Kanisa la Mungu, *"alilolinunua kwa damu yake mwenyewe"* (Mdo 20:28).

Kazi ya Kristo msalabani ni kwa sababu ya upendo wa Mungu

Katika 1 Yohana 3:5 tunasoma kwamba, *"Nanyi mnajua ya kuwa yeye alidhihirishwa, ili aziondoe dhambi; na dhambi haimo ndani yake"* (tazama pia Mt 1:21). Wakati Kristo alipojitoa kama sadaka ya upatanisho hakuwa sawa na mtu anayejaribu kumtuliza Mungu ambaye ni mkali kwa kumpa zawadi. 1 Yohana 4:10 inatuambia kwamba sadaka ya Kristo ilikuwa tendo la Mungu mwenyewe lililoonesha upendo wake. Zawadi hii ya Kristo ilitolewa kwa sababu ya upendo wa Mungu (Rum 5:8; 8:32; Yn 3:16).

Mungu hana upendeleo, tuitangaze Injili kwa wote

Yesu Kristo alikufa, si kwa dhambi zetu tu, lakini vilevile, *"Kwa dhambi za ulimwengu wote."* Tendo hili ni uthibitisho kwamba Mungu hana upendeleo kwa mtu ye yote. Sadaka ya upatanisho imetolewa kwa watu wote duniani. Jambo hili linapasa kutukumbusha wajibu wetu wa kuifikisha Habari Njema kwa wote wanaopotea bila Kristo.

Dhambi huleta mauti

Adhabu au hukumu ya maisha ya dhambi inaonekana katika 1 Yohana 5:16. Kwa mtoto wa Mungu kuna dhambi inayoleta mauti ya mwili tu. Mstari huu hautaji dhambi fulani lakini bila shaka ni hali ile ya kuendelea katika dhambi. Kuendelea kufanya dhambi ni kufanya *"dhambi iliyo ya mauti"* kwa sababu dhambi huleta mauti (Yak 1:15). Kuendelea katika dhambi haitakiwi kwa Mkristo. Inaonekana Mkristo akiendelea katika dhambi, Mungu ana-

weza kumwondoa duniani na kumpeleka mbinguni ili asiendelee katika dhambi zake. Kwa mtu asiyeamini Yesu Kristo, dhambi huleta mauti ya mwili na pia ya kiroho milele.

Kuungama huleta msamaha, baraka, na ukaribu na Mungu

Yohana 1:9 inasema, *"Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kututakasa na udhalimu wote."* Kwa sababu ya neema na upendo wa Mungu, Mkristo anaweza kuziungama dhambi zake na kupokea baraka ya kusamehewa na kusafishwa. Kuungama dhambi kwa Mkristo ni kuitambua dhambi yake na kuitaja wazi-wazi mbele ya Mungu sawa na jinsi Daudi alivyofanya (Zab 32:5; 51:3). Ni kukiri au kukubaliana na Mungu kuhusu dhambi yake ilivyo. Zoezi la kuiungama dhambi linapaswa kufanyika kila mara dhambi inapotendeka. Kwa Mkristo anayeitambua hali ya dhambi yake, haiwezekani kwake kuendelea hata siku moja bila kuiungama dhambi yake kwa Mungu. Roho Mtakatifu anamsaidia Mkristo anapohakikisha rohoni mwake kwamba ametenda dhambi. Kazi ya Roho Mtakatifu ni kumsaidia Mkristo kutambua dhambi zake ili azichukie, aziungame, na aachane nazo.

<u>Maana Kwetu Leo</u>

1. Yohana anataka wasomaji wake kujiepusha na dhambi. Katika sura ya kwanza anafundisha mambo gani yanayopaswa kutuongoza kuishi maisha ya utakatifu?

2. Kwa vile mimi ni Mkristo na dhambi zangu zimesamehewa, nikitenda dhambi au nisipotenda dhambi, kuna nini?

3. Wakati ninapofanya dhambi, Bwana Yesu ananisaidiaje katika maisha yangu?

4. Kuungama kunasaidiaje mimi kurudishiwa ushirika na Mungu? (tazama pia Mit 28:18; Yak 5:16).

5. Unaweza kufanya dhambi bila kusikia uchungu moyoni mwako? (tazama pia Isa 5:12-13; Yer 2:35).

6. Kuna nini katika maisha yako kinachozuia ushirikiano wako na Mungu katika kusoma Neno la Mungu na kuomba? (k.m. 2 Tim 2:4; Mk 12:29-30).

7. Maandiko haya yanataja dhambi mbalimbali (1 Tim 1:6-11; 6:4-20; 2 Tim 3:1-5; Tit 1:7; 3:3; 2 Kor 12:20; Gal 5:19-21; Rum 1:28-32; 3:13-19; 13:13; 1 Kor 5:10-11; 9:12). Kati ya dhambi zilizotajwa katika mistari hii, je, kuna moja au zaidi ya dhambi hizo katika maisha yako? Kama jibu lako ni ndiyo tumia muda huu sasa hivi kuomba na kuungama dhambi hizo kwa Mungu. Sasa, kwa vile umekiri dhambi hii (au hizi) kwa Mungu na kusafishwa kwa damu ya Kristo, sikia maneno haya: *"Mmesamehewa dhambi zenu, kwa ajili ya jina lake"* (1 Yn 2:12). Nenda kwa amani na umtumikie Mungu na mikono safi na moyo mweupe.

Mistari Mikuu

1 Yohana 2:1-2; 1:9 – "Watoto wangu wadogo, nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki, naye ndiye kafara ya upatanisho wa dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu, bali na kwa dhambi za ulimwengu wote - Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kututakasa na udhalimu wote."

FUNDISHO #4 - KUWALINDA WATAKATIFU WA MUNGU

Yohana aliandika waraka wake wa kwanza akiwa na makusudi mbalimbali. Kusudi la kwanza lilikuwa kuonesha wazi ushirika wetu; la pili lilikuwa kuongeza furaha yetu; na la tatu kuzuia dhambi. Kusudi la nne ni kuwalinda watakatifu wa Mungu.

Mungu ameionya jamii ya Kanisa (watoto wadogo) juu ya mashindano yaliyo kati ya nuru na giza (1:1-2:6) na kati ya upendo na chuki (2:7-11). Sasa anawaonya juu ya mashindano ya tatu yaliyo mashindano kati ya ukweli na uongo. Haitoshi kwa muumini kutembea katika nuru na kutembea katika upendo; anapaswa vilevile kutembea katika ukweli.

Mtume Yohana anaangalia sehemu tatu katika kulielezea jambo hili la ukweli. Katika sehemu ya kwanza anaeleza tofauti iliyopo kati ya walimu wa uongo wa siku zile na watoto wa kweli wa Mungu (2:18-21). Katika sehemu ya pili anaeleza maana ya uzushi (mafundisho yasiyo kweli) yaliyofundishwa na wapinga Kristo (2:22,23). Katika sehemu ya tatu anawatia Wakristo moyo kujikinga na mafundisho ya uongo kwa kuzitumia silaha mbili zenye umuhimu mkubwa katika mashindano haya, ndiyo kweli ya Habari Njema na Roho Mtakatifu (2:24-27).

Mashindano na walimu wa uongo

Tuangalie namna Yohana anavyoonesha tofauti iliyopo kati ya walimu wa uongo na Wakristo wa kweli (2:18-21). Kwanza anawaarifu kuwa wamo katika *"wakati wa mwisho"* na kwamba *"wapinga Kristo wengi wamekwisha kuwapo."* Maneno haya yanaonesha wazi kwamba Wakristo wanaishi katika wakati wa hatari na kwa sababu hii wanapaswa kujilinda na makosa yanayoletwa na adui zao.

"Wakati wa mwisho" unaonesha kwamba wakati mpya umeanza duniani na *"giza linapita na ile nuru ya kweli imekwisha kung'aa"* (2:8). Tangu kufa na kufufuka kwa Bwana Yesu, Mungu amefanya "kitu kipya" katika dunia hii. Historia ya Agano la Kale ilikuwa inatutayarisha na kutufikisha kwa *"wakati wa mwisho."* Ukomo wa *"wakati wa mwisho"* utakuwa wakati Bwana Yesu atakaporudi na kusimamisha ufalme wake. *"Wakati wa mwisho"* ulianza katika siku za Yohana na unaendelea hata leo. Katika siku za Yohana kulikuwa walimu wa uongo na hata leo wanaendelea kuongezeka tu. Paulo anaeleza habari ya *"Wakati wa mwisho"* katika 1 Timotheo 4 na 2 Timotheo 3. Sisi Wakristo wa Daraka la Neema tutanyakuliwa kwenda mbinguni kabla ya kipindi cha Dhiki Kuu na kabla Bwana Yesu hajarudi kuihukumu dunia na kuusimamisha ufalme wake. Tuseme, *"wakati wa mwisho"* una muda mrefu usioeleweka. Yohana hajatoa kipimo cha wakati huo bali ameeleza zaidi hali na tabia yake.

Sisi Wakristo wa leo tunaishi katika *"wakati wa mwisho"* na tunapaswa kutambua ni siku za hatari. Kwa sababu hiyo ni lazima tuyajue yale tunayoyaamini na kwa nini tunayaamini.

Maneno, *"mpinga Kristo,"* yanatumiwa katika maandiko ya mtume Yohana peke yake (1 Yn 2:18,22; 4:3; 2 Yn 7), lakini wazo la *"mpinga Kristo"* linafundishwa katika vitabu vingine vya Neno la Mungu. Maandiko ya Agano la Kale, vitabu vya Injili, na barua za mtume Paulo vinafundisha juu ya watu hawa wakiitwa *"watu wa dhambi."* (Linganisha 2 Thes 2:4 na Dan 11:36-37; Ufu 13:1-8 na Dan 7:8,20; 8:24; 11:28-30. Soma vilevile Eze 38-39; Zak 12-14; Mt 24:4,5,11,14,24; Mk 13:22; 2 Thes 2:1-12 na Ufu 17:8). Maana ya maneno *"mpinga Kristo"* ni mwenye kumpinga Kristo au mwenye kusimama kinyume na Kristo.

Walimu hawa wa uongo (ambao wanaitwa wapinga Kristo) walikuwa wakijaribu kuwadanganya Wakristo (2:26), kuwapeleka pembeni, na kuwatoa kutoka katika ushirika wa Kanisa la Kristo. Waovu hawa walikuwa watu waliojiunga na Kanisa, lakini mwishoni walionekana kuwa ni watu ambao hawakuzaliwa na Mungu kweli (2:19). Kwa uasi wao, walithibitisha kwamba hawakuwa watu waliomo ndani ya Mwili wa Kristo. Yohana anafundisha kanuni inayosema kwamba walio wa kwetu watabaki nasi (2:19). Kuendelea hata mwisho ni alama ya kwamba tumeungwa na Kristo kweli (Ebr 3:14).

a. Taja mambo yanayosemwa juu ya watoto wa Mungu katika 1 Yohana 2:20-21.

Mafundisho ya walimu wa uongo

Yohana anaendelea akieleza mafundisho ya uongo ya wapinga Kristo (2:22-23). Walimu hawa walikuwa wakiyakana mafundisho gani ya kweli?

- Walikana kwamba Yesu ni Kristo na Mwana wa Mungu (2:22).
- Walikana kwamba Kristo alikuja katika mwili (4:2; 2 Yn 7).
- Waliyakana mamlaka na maagizo ya Yesu (2:4).
- Walikana hali yao ya kuwa ni wenye dhambi (1:8,10).
- Walikana kwamba wokovu ni katika Kristo tu (2:2).
- Walikana agizo la waumini kupendana (2:9).
- Walikana kwamba mwenendo wa haki ni lazima katika kushirikiana na Mungu (1:6; 2:29; 3:6,10).
- Walikana wajibu wa kuishi kama Yesu alivyoishi (2:4,6; 3:7).
- Walikana hali ya ushirika kati ya waumini, Baba, na Mwana, na hata kati yao kama waumini (1:3; 2:11).
- Waliyakana mamlaka ya Yohana kama mtangazaji wa habari iliyokuwa tangu mwanzo (1:5; 3 Yn 10).
- Walikana kwamba wasiowafuata wao ni Wakristo wa kweli (2:20-21).

Kosa la msingi la walimu hawa lilikuwa kukana kwamba Yesu ni Kristo. Walikana hali ya Yesu kuwa Mungu na binadamu wakati mmoja. Yohana anasema mafundisho yao ni ya uongo na hata wao wenyewe ni waongo (2:22). Mstari wa 23 unatufundisha kuhusu umoja kati ya Baba na Mwana; lakini zaidi ya hii, inatufundisha kwamba kumkana Mwana ni kujitenga na Baba.

Yohana anafundisha matokeo ya mafundisho ya uongo huwa ni mabaya sana. Yohana anasema kwamba kumkana Mwana ni kumkana Baba. Vilevile kumkana Yesu kuwa Mungu ni kumkana Mungu. Yohana anasema wanaomkana Yesu wanajitenga na Mungu katika maisha yao. Yohana anatumia maneno haya, *"sisi tu wa Baba."* Maana yake ni kwamba yule asiyemkiri Yesu kuwa ni Kristo na Mungu anabaki katika hali ya upotevu na anaingojea hukumu ya Mungu.

Udanganyifu ni ishara kubwa ya *"wakati wa mwisho"* (Mt 24:3-5,11,23-24). Kwa sababu hii Wakristo wanapaswa kujikinga na walimu wa uongo na mafundisho yao ya uongo. Wakristo wanawezaje kujikinga na kujilinda na mafundisho haya ya uongo? Jibu la Yohana ni kwamba Wakristo wanapaswa kuzitumia silaha kubwa mbili walizopewa na Mungu (2:24-27) ili Kanisa lisipelekwe pembeni na walimu wa uongo.

Silaha ya kwanza ya Wakristo ni Neno la Mungu. Wanapaswa kukaa katika habari ile ya kweli waliyoisikia kutoka mwanzo (1:1; 2:7,12,24; 3:11). Mafundisho yote ya Neno la Mungu yanapaswa kuwa na makao mioyoni mwao. Vilevile Wakristo wanapaswa kulikubali Neno la Mungu likae ndani yao ili liwaongoze na kuwajenga. Hawapaswi kulidharau wala kuliacha Neno la Mungu na kuyafuata mafundisho mapya ya uongo.

b. Mtume Paulo anasema kwamba Wakristo wanapaswa kufanya nini? (2 Tim 3:14-17)

Silaha ya pili ni Roho Mtakatifu. Wakristo wana silaha hii na walimu wa uongo hawana. Roho Mtakatifu ndiye anayefundisha Wakristo kupitia Neno la Mungu lililo hai. Yohana anamtaja Roho Mtakatifu kama mafuta yaliyomiminwa (2:20,27).

Mafundisho ya Neno la Mungu ni haya kuhusu kazi ya Roho Mtakatifu: Mungu humweka Roho Mtakatifu katika muumini wakati anapozaliwa mara ya pili (2 Kor 1:21-22; Gal 3:2, 1 Yn 3:24; 4:13). Vilevile, Roho Mtakatifu anamweka muumini yule katika Mwili wa Kristo (1 Kor 12:13), yaani kwa kumbatiza katika Kristo. Kuanzia saa ile ya kuokolewa, Roho Mtakatifu anakaa katika muumini na muumini anakaa katika Kristo.

Katika mstari wa 2:27 tunasoma kwamba Roho Mtakatifu anakaa ndani ya waumini (Katika Biblia ya Kiswahili neno linalotumiwa hapa ni *"mafuta"* lililo mfano wa Roho Mtakatifu). Wakati Yohana anaposema Roho Mtakatifu anakaa ndani ya Wakristo anaonesha kwamba kukaa kwake si kwa muda tu, bali, kwa hakika, anabaki katika mioyo yao hata milele. Habari hii inatupa sisi Wakristo uhodari kwa kuwa inatupa uhakika kuhusu wokovu wetu. *"Kukaa"* katika Kristo ni kuungwa naye na kushirikiana naye pia. Neno la Mungu linasema sisi ni katika Kristo na hivyo linatusihi kumtegemea Kristo kutuwezesha katika maisha yetu ya Kikristo.

Jambo la Roho Mtakatifu kukaa ndani yetu linatupatia uwezo wa kufahamu mambo ya kiroho (2:20,21,27). Wakristo, kwa njia ya Roho Mtakatifu kukaa ndani yao, wanatiwa nuru. Wakati Yohana anapoandika kwamba Roho Mtakatifu anatufundisha *"mambo yote,"* maana yake ni kwamba sisi Wakristo tunajua mambo yote yanayohitajika kwa ajili ya wokovu. Mafundisho haya hayahitaji nyongeza kutoka kwa walimu wa uongo. Kwa njia ya Roho Mtakatifu anayekaa ndani yetu, tuna mbinu wa kulifahamu Neno la Mungu sisi wenyewe. Tena tunaweza kulitumia katika mashindano yetu na walimu wa uongo tukijikinga na mafundisho yao ya uongo.

c. Roho Mtakatifu anatusaidia kwa njia gani wakati tunaposoma Neno la Mungu? (Tazama pia 1 Kor 2:10-16)

<u>Maana Kwetu Leo</u>

1. Mafundisho gani ya msingi kuhusu Kristo na Mungu yanakanushwa na walimu wa uongo?

2. Tabia hii ya kukanusha mafundisho inaonekana leo katika kanisa au nchi yako? Namna gani?

3. Kwa nini ilikuwa lazima Yesu afanywe kuwa mwanadamu mkamilifu yaani wa kweli?

4. Andika hapa chini yale 1 Yohana 4:1-6 yanayofundisha juu ya roho ya kweli na roho ya uongo (soma vilevile Yn 14:17; 15:26 na 16:13).

Roho ya kweli -

Roho ya udanganyifu -

5. Wakristo waliozaliwa mara ya pili wanapaswa kufanya nini dhidi ya *"wapinga Kristo"* wanaofundisha elimu za uongo?

6. Alama za utii, upendo na kweli zinaonekana namna gani katika maisha yako? (Soma 2 Kor 13:5)

Mistari Mikuu

1 Yohana 2:20,27 – "Nanyi mmepakwa mafuta na Yeye aliye Mtakatifu nanyi mnajua nyote. . . Nanyi, mafuta yale mliyoyapata kwake yanakaa ndani yenu, wala hamna haja ya mtu kuwafundisha; lakini kama mafuta yake yanavyowafundisha habari za mambo yote, tena ni kweli wala si uongo, na kama yalivyowafundisha, kaeni ndani yake."

FUNDISHO #5 - KUTANGAZA MSAMAHA WA DHAMBI

Tangazo la msamaha wa dhambi ni kusudi la tano la kuandikwa kwa waraka wa 1 Yohana. Mtume Yohana aliandika ili aitangaze Habari Njema ya kwamba dhambi za watu zinaweza kusamehewa na Mungu.

Haiwezekani kwa mtu kuwa Mkristo isipokuwa dhambi zake zimesamehewa. Kama mtu yumo ndani ya Kristo kwa njia ya kumwamini Yesu Kristo, dhambi zake zimeshahukumiwa na Mungu katika kazi ya Yesu Kristo msalabani. Matangazo ya kusamehewa dhambi kwa njia ya kumwamini Kristo ni Habari Njema ya Injili (Mdo 13:38).

Lakini, haitoshi kwa mtu kuamini kwamba dhambi zinaweza kusamehewa. Watu wengi wamezoea kusema, "Ninaamini kuna msamaha wa dhambi," lakini wenyewe siyo Wakristo. Kuamini tu kwamba kuna msamaha wa dhambi hakuwezi kumletea msamaha wa dhambi na kumfikisha mtu mbinguni. Lazima aombe msamaha wa dhambi katika maisha yake, kwani msamaha ni baraka kubwa ya kiroho ambayo tunapaswa kuipokea (Efe 1:3,7).

Kama tulivyokwisha kusema tayari, kusudi moja la Yohana katika kuandika barua hii ni kuutangaza msamaha wa dhambi. Tujifunze juu ya jambo hilo kwa kufuata mafungu haya. (1) Msamaha ni baraka kamili; (2) Msamaha ni baraka kwa anayepokea; na (3) Msamaha ni baraka inayozaa matunda.

Msamaha ni baraka Kamili

Mtu mwenye dhambi anapomwamini Yesu, anapatanishwa na Mungu. Baraka ya kwanza inayopatikana kwake ni dhambi zake zote kusafishwa - yaani, kusamehewa. Baraka zote za kiroho zinazuiliwa mpaka mtu anapoupokea msamaha wa dhambi. Kutosamehewa ni kuendelea kuishi chini ya hasira na hukumu ya Mungu. Asiyesamehewa hapewi baraka za kiroho.

Tunapotazama 1 Yohana 2:12, tunasoma kwamba *"mmesamehewa dhambi zenu."* Sarufi ya neno *"mmesamehewa"* inahusu wakati uliopo katika maisha ya Mkristo. Katika maisha ya Mkristo, tendo la msamaha limefanyika katika muda uliopita lakini faida ya msamaha huo inaendelea katika muda uliopo wa Mkristo huyu. Yaani, mstari huu unaeleza hali ya Mkristo kuwa mtu aliye na msamaha nyakati zote baada ya kusamehewa kwa kuwa msamaha wake ni wa hali timilifu. Msamaha wa Mungu kuhusu dhambi zote za mtu ni kamili na unadumu.

Dhambi zililipiwa malipo kamili msalabani. Yesu aliondoa dhambi kabisa kwa ajili ya wote wanaomjia Mungu kwa njia ya imani katika Yesu Kristo. Wote hawa wanaomwamini Yesu wanasamehewa dhambi zao hata milele. Waumini wote wanaweza kusema, "Nina msamaha wa dhambi" (Efe 1:7; Kol 1:14).

Msamaha ni uthibitisho halisi wa wokovu unaookoa watu na hukumu ya dhambi. Msamaha halisi ni huu - *"Mungu katika Kristo aliwasamehe ninyi"* (Efe 4:32).

Msamaha ni baraka ya mtu anayepokea

1 Yohana 2:12 inaendelea kusema, *"Mmesamehewa dhambi zenu kwa ajili ya jina lake."* Sisi wenye dhambi tunapata msamaha kumpitia Kristo asiyefanya dhambi. Kristo alikufa kwa ajili yako na kwa ajili yangu akihukumiwa kwa ajili ya dhambi zetu sisi sote. Ingawa Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi za watu wote duniani, si wote watakaosamehewa dhambi zao. Ni lazima kila mmoja amwamini Yesu na kazi yake aliyomfanyia msalabani. Kwa njia hiyo atapata msamaha wa dhambi zake kwa maana Mungu atakubali kumhesabia malipo ambayo Yesu Kristo alimlipia deni lake.

Kuna jambo moja lililo gumu ambalo halieleweki vizuri kwetu kuhusu msamaha. Neno la Mungu linafundisha kwamba Mungu hawezi kuwahurumia wenye dhambi kana kwamba ameamua dhambi si kitu cha kukihukumu. Yaani, wenye dhambi hawasamehewi kwa sababu tu ya huruma au uzuri wa roho ya Mungu. Mungu anawasamehe watu kwa njia ya msalaba tu, yaani, kwa njia ya kuzihukumu dhambi za watu ndani ya Yesu. Dhambi ni kitu kikubwa kwake Mungu mwenye haki na badala ya kuisahau tu au kuihesabu si kitu, ilikuwa lazima aihukumu. Sisi, tuliomwamini Yesu, tunasamehewa kwa sababu dhambi zetu zilihukumiwa katika Bwana Yesu wakati alipokufa msalabani. Haya ni mafundisho ya 2 Wakorintho 5:21: *"Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika yeye."* Bwana Yesu aliweza kuulipa mshahara wa dhambi kwa sababu yeye hakuwa mwenye dhambi. Wakati mimi ninapopokea msamaha wa dhambi, kwa kumwamini Yesu, baraka ya Mungu inanifikia mimi binafsi kwa sababu nilimkubali Kristo na kumwamini. Watu wote ambao hawajasamehewa dhambi zao, hawajasamehewa kwa sababu hawajamwamini Yesu. Ni lazima kila mmoja amwamini Yesu na ndipo atapewa msamaha.

Msamaha ni baraka inayozaa matunda

Msamaha unaufurahisha moyo. Tunaposamehewa tunawekwa huru na hukumu (Rum 1:8). Hivi woga wa kufa na woga wa hukumu umeondolewa. Hakuna furaha kubwa duniani kuliko kuwa na uhakika wa msamaha wa dhambi. Msamaha huo wa kuikwepa hukumu, ambayo tumekuwa tukiiongelea katika aya zilizotangulia, unamhusu mpotevu anapomwamini Bwana Yesu (1 Yn 2:12; Efe 1:7; 4:32; Kol 1:14; 2:10-14).

Lakini tusisahau kwamba Wakristo wanahitaji msamaha wa dhambi zao wanazozitenda baada ya kuokoka vilevile. Si kwamba wako chini ya hukumu ya Mungu tena, hapana. Maana, wameshasamehewa dhambi zao zote; zilizotendeka, zinazotendeka, na zitakazotendeka. Msamaha huo waliopewa siku ya kuokoka ni msamaha utokao kwa Mungu kama hakimu. Mahakamani mwa Mungu, Mungu anatangaza msamaha kwa kila moja anayemwamini Yesu. Isitoshe, kama hakimu, anawatangazia wanaomwamini Yesu kuwa wamevalishwa haki ya Yesu na hivyo wanaitwa watakatifu wenye haki. Msamaha huo unawaondoa kutoka katika hukumu na unahusu dhambi zao zote ikiwa ni pamoja na dhambi ambazo bado hawajazitenda. Matokeo ya msamaha huo ni kufanywa kuwa watoto wa Mungu na kuingizwa katika familia ya Mungu wakihusiana na Mungu kama Baba na mwana.

Sasa, kama wana wa Mungu, kila Mkristo ana uwezo wa kutenda dhambi mara kwa mara, ingawa ameagizwa kutotenda. Dhambi hizo zinatendeka na Wakristo wakiwa watoto wa Mungu. Zimeshasamehewa mahakamani mwa Mungu lakini bado zinaathiri uhusiano wao na Mungu kama Baba yao katika familia moja (ingawa haziathiri kiasi cha kupoteza wokovu wala kutohesabika kuwa watoto wa Mungu tena). Kwa maneno mengine, dhambi zinazotendwa na Wakristo zinavunja ushirikiano wao na Mungu, Baba yao. Wakristo wanaokosa furaha ni wale wasioshirikiana na Mungu kwa ukaribu kwa sababu ya kuwepo kwa dhambi maishani mwao. Ni lazima kwa Mkristo kuziungama dhambi zake ili zisamehewe na zisafishwe. Ndiyo maana ya 1 Yohana 1:9 tunaposoma habari kuhusu msamaha unaopatikana kwa watoto wa Mungu wanapoziungama dhambi zao. Msamaha wa mahakamani mwa Mungu ulitendeka siku Mkristo alipomwamini Yesu. Lakini baada ya kuokoka, msamaha wa kifamilia unaendelea kuhitajika wakati Mkristo anapotenda dhambi mara kwa mara.

Tunapaswa kutofautisha aina hizi mbili za msamaha. Aina ya kwanza ni msamaha wa dhambi katika wokovu, wakati wa kumwamini Bwana Yesu, kufanywa wana wa Mungu, na kuingizwa katika jamii ya Mungu. Msamaha huu unafanyika mara moja tu - siku ya kuzaliwa mara ya pili. Lakini kuna msamaha wa namna nyingine - Msamaha katika jamii ya Mungu. Msamaha huu ni kwa ajili ya watu walio Wakristo tayari, yaani kwa ajili ya watoto wa Mungu. Msamaha huo unapatikana wakati Wakristo wanapoziungama dhambi zao kwa Mungu aliye Baba yao. Kusudi la msamaha huo ni kuboresha uhusiano wao wa kifamilia (yaani si msamaha katika uhusiano wao na Mungu kama hakimu kwa kuwa msamaha huo umekamilika tayari). Wakati Wakristo wanapoziungama dhambi zao, Mungu anawasamehe na ushirika wao na Mungu unarudishwa katika hali nzuri. Mkristo anayeishi katika dhambi

hana ushirika mzuri na Mungu. Kwa sababu hii Yohana anatusihi kuungama dhambi zetu kwa Mungu (1:9).

Kumbuka kwamba kuna msamaha wa wokovu na msamaha wa jamii (ushirika). Tukiyafahamu mambo hayo tutaweza kuona kwamba andiko la 1 Yohana 1:9 halipingi andiko la 1 Yohana 2:12. 1 Yohana 2:12 inafundisha msamaha unaopatikana katika siku ya wokovu. Huu ni usafisho wa kuzaliwa mara ya pili. 1 Yohana 1:9 inafundisha msamaha wa siku hadi siku unaoturudishia ushirikiano na furaha yetu na Mungu pamoja na kuleta amani katika jamii ya Mungu. Huu ni usafisho wa utakaso.

a. Maana ya neno "Kusamehe" ni "kutupilia mbali." Neno hili linafundishwa namna gani katika Walawi 16:7-22?

Maana ya maneno "kuungama" au "kukiri" ni "kukubali au kusema sawasawa na mwingine." Kukiri kwa Mungu ni jambo linalofanywa na muumini akitambua dhambi yake na kuitaja waziwazi mbele ya Mungu kama Daudi alivyofanya (Zab 32:5; 51:3). Mungu anaelewa makosa ya mwenye dhambi tayari hivyo kuungama dhambi si kumtaarifu Mungu habari mpya kwake. Bali, Mkristo anapokiri au kuungama dhambi yake ina maana anatambua dhambi aliyoitenda na anaelewa hali halisi ya dhambi ile kuwa ni uovu kama vile Mungu anavyoielewa. Tuseme anayekiri anakubaliana na Mungu kuwa amefanya dhambi na kwamba dhambi ile ni mbaya.

Katika baraka ya msamaha kuna onyo kwetu sisi kusameheana. Jambo moja linaloonesha hali yetu mbele ya Mungu ni jinsi tunavyowatendea watu wanaotukosea au kutuumiza. Unawatendea vipi watu wanaokukosea katika maisha yako? Je, unawatendea kwa hasira au kwa kulipiza kisasi? Je, unawatendea kwa kunung'unika? Ikiwa sisi tunafahamu namna Mungu anavyotutendea sisi wakati tunapokosa na kukiri makosa yetu, basi sisi vilevile tutawasamehe wale wanaotukosea au kutuumiza.

b. Agizo la kusameheana linaandikwa katika Waefeso 4:32 na Wakolosai 3:12-13. Maana ya kusameheana ni nini?

Kama Wakristo tunapaswa kuwasamehe wengine kwa sababu Mungu ameshatusamehe sisi. Wakati sisi tulipomkosea Mungu yeye hakutuhukumu. Bali kwa huruma alimtuma Mwana wake kufa kwa ajili ya dhambi zetu ili atupatanishe naye. Kwa sababu Mungu ametutendea hivyo, sisi vilevile tunapaswa kuwasamehe wengine.

Yesu alikaza jambo hilo kwa wanafunzi wake aliposema, *"Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi"* (Mt 6:14-15). Ni lazima kwa mtu anayesamehewa kuwasamehe wengine.

c. 2 Wakorintho 2:10-11 inatoa mfano gani kuhusu jambo hilo?

Mungu anatuamuru kusameheana. Agizo hili linatufundisha mambo haya:

- Msamaha ni lazima. Wale waliosamehewa wanaambiwa wawasamehe wenzao pia. Kushindwa kufanya hivyo ni kuasi agizo la Bwana (Lk 17:3-4).
- Msamaha unapaswa ufanywe kwa moyo safi na kwa moyo wote (Mt 18:35).
- Yeye anayemsamehe mwingine anapaswa kumrudisha na kumsaidia ayashinde matendo yake mabaya (Lk 17:3; Gal 6:1).
- Kumsamehe mwingine ni tendo la mapenzi - la kutaka, ijapokuwa moyo haupendi kuifanya. Lazima tumsamehe ndugu kila mara anapotukosea, ijapokuwa mioyo yetu haifurahii kufanya (Mt 18:21-22).
- Kumsamehe mtu mwingine kosa alilolifanya si kusema kosa lile litasahaulika. Kuna mshahara au matokeo ya dhambi. Mtu anaweza kusamehewa pamoja na kuadhibiwa. Maana yake ni kwamba ninapomsamehe mwenzangu kosa lake, ijapokuwa ninalikumbuka, sitatafuta njia ya kumrudishia ubaya.

- Ijapokuwa ndugu anapaswa kutambua kosa lake na kulikiri, Mkristo anapaswa kumsamehe hata kabla hajalitambua na kulikiri. Umuhimu wa kusamehe upo palepale ijapokuwa mkosaji bado hajakiri. Biblia inasema umsamehe aliyekukosea mara moja kusudi usimpe Shetani nafasi ya kukujaribu na kukuangusha katika dhambi.

Jambo la kusameheana kati ya Wakristo ni lazima kwa ajili ya maendeleo (au afya) ya Mwili wa Kristo na kwa ajili ya ushuhuda wa Mwili wa Kristo mbele ya wasioamini. Bila msamaha, uchungu, machukizo, na kuumizana kunaongezeka na Mwili wa Kristo hautaweza kuendelea vizuri katika umoja. Wakati hakuna msamaha, hakuna hamu ya kuwajenga wengine na kuwatumikia.

Lakini, wakati Wakristo wanapokuwa na moyo wa kusameheana, upendo unaongezeka na watu wa Kanisa wanahudumiana kwa amani na mapatano. Umoja huo, ndani ya Kanisa, unakuwa ushuhuda mzuri mbele ya watu na unashuhudia msamaha tulio nao katika Kristo.

<u>Maana Kwetu Leo</u>

1. Maana ya "msamaha" ni nini?

2. Toa mfano wa "msamaha" kutoka Biblia.

3. Toa mfano wa msamaha unaotokana na maisha yako, jinsi ulivyosamehe au kusamehewa.

4. Ni namna gani msamaha wa dhambi unaleta furaha katika maisha yako? (Mt 9:2)

5. Je, unawasamehe wanaokukosea? (Efe 4:31-32; Kol 3:12-13). Kuna mtu unayehitaji kumsamehe leo?

6. Kuna dhambi gani katika maisha yako ambayo unapaswa kuikiri kwa Mungu? (1 Yn 1:9)

7. Maana ya "watoto wadogo" katika 2:12 ni nini?

8. Ni namna gani unaweza kueleza utofauti unaoonekana kati ya 1 Yohana 1:9 na 2:12?

Mistari Mikuu

1 Yohana 1:9 - "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kututakasa na udhalimu wote.

1 Yohana 2:12 – "Nawaandikia ninyi, watoto wadogo, kwa sababu mmesamehewa dhambi zenu, kwa ajili ya jina lake."

FUNDISHO #6 - KUUENDELEZA UPENDO KATI YA WAKRISTO

Hili ni kusudi la sita la mtume Yohana katika kuandika barua yake ya kwanza. Yohana anasema, bila upendo, Mkristo anakosa msingi wa maisha ya Kikristo.

Kabla Yesu hajakamatwa na kuuawa, alikuwepo pamoja na wanafunzi wake. Aliutumia wakati ule kuwafundisha, kuwaonya na kuwafariji. Kwa sababu alijua kwamba muda wake wa kuendelea kuwepo duniani ulikuwa mfupi sana, Yesu alitumia siku zake za mwisho kuwaambia wanafunzi wake maneno yenye umuhimu mkubwa sana kuhusu maisha ya Kikristo. Aliwaambia umuhimu wa kifo chake, kuja kwa Roho Mtakatifu, tumaini la uzima, utumishi wa kuhubiri Habari Njema, na mashindano kati ya dunia na waumini n.k.

Mwishoni Yesu aliwapa wanafunzi wake amri moja tu - wapendane wao kwa wao. Amri hii, inayotajwa katika maandiko mengi ya Agano Jipya, ni msingi wa maisha ya Kikristo, na ni msingi wa amri nyingine zote.

Yesu alisema, *"Amri mpya nawapa, Mpendane. Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo."* Agizo hili, linalotajwa mara ya kwanza katika Yohana 13:34, linaonekana katika maandiko mengine kama yafuatayo: Yohana 15:12-17, Warumi 12:9-10; 13:8, 1 Wathesalonike 3:11-12; 4:9, Yakobo 2:8, 1 Petro 1:22; 3, 1 Yohana 3:11,23; 4:7,11,12,21; na 2 Yohana 5.

Yohana alionesha umuhimu na uzito wa agizo hilo wakati aliposema watu watawatambua wanafunzi wake kwa jinsi wanavyopendana (Yn 13:35). Yaani, ni hali ya lazima kwa Wakristo wote, inapaswa kuwa sifa yao. Baadaye Yohana alikaza umuhimu wa kupendana aliposema wakati mtu hampendi ndugu yake ni ishara ya kwamba hampendi Mungu (1 Yn 4:20).

Agizo hili lina mambo makubwa mawili. 1) Kupendana ni lazima. Wale wanaomwamini Kristo wanapaswa kuwapenda waumini wengine wote. Kukosa kupendana ni kuasi agizo la Bwana Yesu Kristo. 2) Kupendana ni kazi ngumu. Ni lazima Wakristo wajikaze na kujitoa wakimtii Mungu katika agizo hilo la kupendana. Kuna baadhi ya Wakristo wanaokataa kupendana na wengine wanaokubali kupendana. Kukataa ni kuasi. Kukubali ni kutii.

Maneno "upendo/kupenda" yanatajwa zaidi ya mara 50 katika waraka wa kwanza wa Yohana. Waraka huu unautaja upendo mara nyingi zaidi kuliko vitabu vingine vyote vya Agano Jipya kasoro tu Injili ya Yohana. Agizo "mpendane" linaonekana mara tano katika barua hii (3:11,23; 4:7,11,12). Katika maagizo yanayopatikana katika 1 Yohana, agizo hili ni kubwa zaidi kwa sababu linatajwa mara nyingi zaidi.

Mungu ameamuru Wakristo wapendane

(1 Yn 2:3,4,7,8; 3:11,23; 4:7,8,11,12,16,21; 5:1).

1 Yohana 2:7-8 - "Wapenzi, siwaandikii amri mpya, ila amri ya zamani mliyokuwa nayo tangu mwanzo. Na hiyo amri ya zamani ni neno lile mlilolisikia. Tena nawaandikia amri mpya, neno lililo kweli ndani yake na ndani yenu; kwa kuwa giza linapita na ile nuru ya kweli imekwisha kung'aa."

Namna gani amri hii inaweza kuwa ya zamani wakati huohuo ikawa mpya? Kwa upande mmoja ilikuwa ya zamani kwa sababu walikuwa wameisikia ikifundishwa katika vipindi vingine kama vile katika Walawi 19:18, *"Umpende jirani yako kama nafsi yako; Mimi ndimi BWANA."* Mfano mwingine ni wakati ule Yesu alipoulizwa swali juu ya amri ya kwanza iliyo kubwa kuliko amri nyingine zote. Alitaja Kumbukumbu la Torati 6:5, *"Nawe mpende BWANA, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote."* Halafu aliendelea akisema amri ya pili inapatikana katika Walawi 19:18 inaposema, *"Umpende jirani yako kama nafsi yako."*

Lakini kwa upande mwingine, Yohana anasema amri anayowapa ya kupendana ni mpya. Anasema ni mpya kwa sababu wakati Yesu alipofundisha kuhusu upendo alipanua maana yake. Yesu aliweka uzito zaidi katika upendo na maisha yake yalikuwa mfano kamili wa upendo ambao aliufundisha.

Upya wa amri hii unaonekana pia kwa walengwa wa upendo. Wengi walihesabu upendo kuwa lazima kwa watu fulani tu, si kwa wote. Watu waligawanywa katika vikundi.

Kulikuwa na vikundi vilivyostahili kupendwa na vikundi vingine hapana. Vikundi vilivyofikiriwa vilikuwa kama vile familia, marafiki, watu wa taifa moja, au hata wenye dhambi na wasio wenye dhambi. Wayahudi hawakuona ni lazima kuwapenda wenye dhambi kwa kuwa walistahili tu hukumu ya Mungu. Vilevile Wayahudi hawakuamini ni lazima kuwapenda watu wa mataifa mengine. Lakini Yesu aliwafundisha kitu tofauti na mawazo hayo. Yesu alifundisha kwamba watu wote wanastahili upendo. Fundisho hilo linapatikana katika fundisho la Yesu ndani ya mfano wa Msamaria Mwema unaofundisha jirani ni mtu ye yote anayemjali ye yote mwenye mahitaji (Lk 10:29-37). Yesu mwenyewe alikuwa mfano wa fundisho hilo katika matendo yake, kama vile alivyokula na watoza ushuru na makahaba.

Vilevile upya wa amri hii unaonekana katika ufafanuzi bora uliotolewa na Yesu kuhusu upendo. Upana na urefu wa upendo wa Mungu ulioneshwa msalabani. Mtu wa Mungu anapaswa kuwapenda wengine, si kwa kadiri tu ya jinsi anavyojipenda, bali kwa kufuata mfano wa upendo ambao Yesu aliuonesha; upendo wa kujitoa hata kufa msalabani.

Amri hii inaelezwa zaidi tunapoangalia maana ya upendo. Katika barua hii tunasoma mara mbili, *"Mungu ni upendo"* (4:8,16). Fikiria maana ya maneno haya. Hayasemi tu kwamba Mungu ni mwenye upendo wala upendo ni tabia ya Mungu (ingawa maana hizo pia ni kweli). Bali maneno haya yaonesha kwamba upendo ni sehemu ya asili ya Mungu; jinsi alivyo. Upendo wote wa kweli, wema, na huruma unatoka kwake Mungu. Bila Mungu hakuna upendo. Upendo ni kanuni ya milele inayotokana na asili yake. Haiwezekani upendo ukakosekana katika utu wake kwani yeye ni upendo. Tunapoelewa Mungu ni upendo ndipo tunaweza kuelewa vizuri zaidi kwa nini watoto wa Mungu wanapaswa kupendana.

a. Upendo wa kweli ni nini katika ufafanuzi wa mistari ifuatayo?

Warumi 15:2 -

Warumi 13:8-10 -

1 Wakorintho 13:1-8, 13 -

Upendo wa Mungu na Yesu unatufundisha maana ya upendo

(1 Yn 3:16; 4:10)

Je, umeona kwamba tuna Yohana 3:16 mbili? Yohana 3:16 na 1 Yohana 3:16 zinafundisha kitu kimoja. Mateso ya Yesu msalabani yalionesha ukubwa wa upendo wa Mungu na wa Yesu vilevile. Isitoshe, tendo hilo la kufa msalabani kwa ajili ya watu wenye dhambi, lilifafanua maana yenyewe ya upendo.

Tazama 1 Yohana 3:16, *"Katika hili tumelifahamu pendo, kwa kuwa yeye aliutoa uhai wake kwa ajili yetu; imetupasa na sisi kuutoa uhai wetu kwa ajili ya hao ndugu."* Mstari huu unatufundisha maana ya neno upendo. Unasema tunapata kufahamu maana ya upendo tunaposhuhudia tendo la Yesu la kujitoa kwa ajili yetu msalabani. Ni vigumu kuufahamu upendo kwa kutumia maneno tu. Upendo unaeleweka hasa tunapooneshwa mifano ya matendo yake. Watu wanauelewa zaidi upendo, wanapooneshwa upendo na mtu mwingine. Yaani, watu wanapoonja hali ya kupendwa ndipo wanaanza kuuelewa upendo vizuri zaidi.

Tulishasema Mungu "ni" upendo na upendo wote huanzia kwake. Watu wanaompokea Yesu kama Mwokozi wao ni wenye kufahamu maana ya upendo. Hii ni kwa sababu wameelewa jinsi Yesu na Mungu walivyowapenda wakati Yesu alipoadhibiwa msalabani kwa ajili ya dhambi zao. Hao ndio wamejitambua kuwa wakosaji wasiostahili kupendwa, lakini, pia, wameonja upendo wa ajabu wa Mungu, na kwa jinsi hii wamejifunza kuhusu upendo wa kweli.

Upendo wa Mungu ulioneshwa msalabani wakati Kristo alipokufa, maana, *"Aliutoa uhai wake kwa ajili yetu"* (3:16). Msingi wa upendo, yaani maana yake halisi, ni katika neno *"kujitoa"*. Kujitoa ni tendo la upendo lilionekana katika Bwana Yesu na linapaswa sasa kuwa tabia yetu sisi Wakristo.

Mstari wa 16 unaendelea kusema kwamba, *"Imetupasa na sisi kuutoa uhai wetu kwa ajili ya hao ndugu."* Tunaambiwa kwamba TUNAPASWA kufanya hivyo. Ni sharti la Kikristo kwa sababu sisi ni watu wa Kristo. Tunapaswa kuufuata mfano wake katika mambo yote na kuishi kama yeye alivyoishi (2:6). Kama upendo wa Mungu kwetu ni mkubwa sana, vivyo hivyo na sisi TUNAPASWA kupendana (4:10).

1 Yohana 4:10 inaeleza zaidi upendo wa Mungu – *"Katika hili pendo la Mungu lilionekana kwetu, kwamba Mungu amemtuma Mwanawe pekee ulimwenguni, ili tupate uzima kwa yeye. Hili ndilo pendo, si kwamba sisi tulimpenda Mungu, bali kwamba yeye alitupenda sisi, akamtuma Mwanawe kuwa kipatanisho kwa dhambi zetu."* Ukuu wa upendo wa Mungu unaoneshwa kwa njia nne:

- Kwanza, ukuu wa upendo wa Mungu unaonekana katika ukubwa wa zawadi ambayo upendo wa Mungu ulitupatia – *"Mwanawe pekee"*. Yohana anatumia jina kamili la Kristo akitaka kuonesha upekee wake. Hakuna mwingine. Kwa kumtuma Kristo, Mungu alionesha upendo mkamilifu ulio mkubwa kwa wenye dhambi, maana alikuwa tayari kumtoa hata mwana wake.
- Pili, ukuu wa upendo wa Mungu unaonekana katika kusudi la kuja kwa Mwana, *"Ili tupate uzima kwa yeye."* Maneno haya yanaonesha tunapewa uzima wa milele kupitia Kristo. Pia yanaonesha upendo wa Mungu kwa kuwa alijitoa kwa manufaa yetu.
- Tatu, ukuu wa upendo wa Mungu unaonekana wazi wakati tunapotambua ni watu gani waliopendwa na Mungu. *"Hili ndilo pendo, si kwamba sisi tulimpenda Mungu, bali kwamba yeye alitupenda sisi."* Msingi wa upendo haupo ndani yetu sisi kumpenda Mungu, bali ndani yake Mungu kutupenda sisi. Ukubwa wa upendo huo unaonekana tunapogundua alitupenda sisi tusiostahili kuupokea upendo wake kwa sababu sisi ni wenye dhambi.
- Nne, ukuu wa upendo wa Mungu unaonekana katika hali ya Kristo kufa kama sadaka. Mungu, *"Akamtuma Mwanawe kuwa kipatanisho kwa dhambi zetu."* Maneno haya yanaonesha kwamba upendo wa Mungu ulikuwa wa bei ghali na ni upendo wa kujitoa kwa ajili ya wenye dhambi.

a. Yesu Kristo alionesha upendo mkamilifu kwetu kwa njia gani?

Flp 2:7 –

Tit 3:14 -

Ebr 7:25 -

Ebr 4:15 -

Ebr 2:18 -

1 Pet 2:24; Rum 5:6 -

2 Pet 3:9 -

1 Yoh 1:9 -

1 Yoh 3:16; Yoh 10:11 -

Yoh 14:2 -

Yoh 10:10 -

Wakristo wapendane wakitumia upendo waliopewa na Mungu

(2:7; 3:1,2,10,11,14,21,23; 4:1,4,6,7; 5:1)

Kwa sababu upendo ni sehemu ya asili na tabia za Mungu, na kwa sababu waumini wamefanywa kuwa washirika wa tabia zake wakati wa kuzaliwa mara ya pili (2 Pet 1:4), basi, tunajua kwamba, *"Pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi"* (Rum 5:5). Hivyo, upendo wa Mungu umo ndani ya watoto wa Mungu kama vile ulivyo ndani ya Mungu.

1 Yohana 3:1 inatuomba kuutazama upendo huu tulio nao – *"Tazameni, ni pendo la namna gani alilotupa Baba, kwamba tuitwe wana wa Mungu; na ndivyo tulivyo. Kwa sababu hii ulimwengu haututambui, kwa kuwa haukumtambua yeye."* Upendo huo ni zawadi tunayopewa na ni yetu hata milele.

Kwa sababu tunafahamu upendo wa Mungu, maandiko yanatusihi tupendane (3:11). Habari Njema haiokoi watu ili waunganishwe na Kristo na waokolewe na hukumu ya Mungu tu. Faida nyingine ya wokovu huo ni jinsi waumini walivyopewa mfano na ufahamu wa upendo ikiwa ni pamoja na uwezo na agizo la kupendana. Yaani wokovu wetu unapaswa kuzalisha matunda ya upendo ndani ya mahusiano yetu. Kwa Yohana, tunapopendana, ni uthibitisho kwamba tumeokoka na sisi ni watoto wa Mungu. Katika 1 Yohana 3:23 kuna mambo mawili ambayo ni amri: Kumwamini Yesu Kristo na kupendana sisi kwa sisi. Imani ya kweli inazaa mwenendo wa kweli.

Wakristo wote wa kweli ni, *"Mwili mmoja katika Kristo, na viungo, kila mmoja kwa mwenzake*" (Rum 12:5), na "*Wenyewe mmefundishwa na Mungu kupendana"* (1 Thes 4:9). Ndivyo Yohana alivyoandika katika barua yake ya pili, mstari wa tano: *"Na sasa, Mama, nakuomba, si kwamba nakuandikia amri mpya, bali ile tuliyokuwa nayo tangu mwanzo, kwamba tupendane."*

a. Tusipopendana tutafanya nini?

Rum 14:13 -

Gal 5:15 –

Gal 5:26 –

b. Lakini tukipendana, tutafanya nini?

Rum 14:19 –

Rum 15:7 -

1 Kor 12:25 -

Gal 5:13 -

Gal 6:2 -

Efe 4:32 -

1 Thes 4:18 -

Ebr 10:24 -

Tunakumbushwa katika 1 Yohana 4:7-8 kwamba yeye asiyeonesha upendo hajamjua Mungu. Ufahamu wa Mungu, ulio wa kweli, unaleta faida katika mwenendo na unaonekana waziwazi katika upendo. Kwa jinsi hii upendo ni kipimo cha kututambulisha kuwa watu wanaomfahamu Mungu. Ukosefu wa upendo unaonesha kwamba hatuna uzima wala ufahamu wa mambo ya kiroho wala uhusiano na Mungu.

*"Kila mtu aaminiye kwamba Yesu ni Kristo amezaliwa na Mungu. Na kila mtu ampendaye mwenye kuzaa, ampenda hata yeye aliyezaliwa na yeye" (*5:1). Kwa sababu kila muumini amezaliwa kuwa mtoto wa Mungu na kwa sababu kila muumini anampenda Mungu aliye Baba wa wote, inawapasa kuwapenda hata wenzao waliozaliwa na Mungu pia.

Namna Wakristo wanavyoweza kupendana

(1:6,8,10; 2:4,6,9; 3:15,16-18; 4:11,19-21)

Jinsi Yesu alivyojitoa ina maana gani kwa ajili ya sisi Wakristo? Mtume Yohana anasema waziwazi kwamba Yesu Kristo ni mfano wetu. 1 Yohana 3:16-18 inasema sisi Wakristo tunapaswa kuutoa uhai wetu kwa ajili ya ndugu zetu. Maana yake tunapaswa kuwa tayari kuingia gharama kwa ajili ya kusaidia watu wengine na hasa waumini wenzetu. Tunaweza kugharimia muda wetu, nguvu zetu, mali zetu, na cho chote kingine kitakachowanufaisha wengine kuliko manufaa yetu sisi wenyewe.

Kawaida hatulazimishwi kujitoa mpaka kufa kama vile Yesu alivyokufa kwa ajili yetu, ingawa katika historia ya Kikristo ni kweli wengine wamejitoa kwa namna hiyo. Mungu anaomba tuwe tayari kuutoa uhai wetu ikilazimika kufuatana na mapenzi yake, lakini kawaida anaomba tujitoe kwa namna mbalimbali tofauti na hali ile ya kujitoa maisha yote hata kufa.

Hakika Mungu anataka Wakristo wote kuwa wafu katika mapenzi yao na kujitoa kwa ajili ya faida ya wengine. Wanapofanya hivyo ni ishara ya kuwemo kwa upendo wa kweli ndani yao. Yesu ametuomba kujikana tukijitwika misalaba yetu na kumfuata (Mk 8:34). Kujikana ni kusema hapana kwa mambo mengi yaliyo katika mapenzi yetu. Wote tunapenda kutimiziwa mahitaji yetu yote, tunapenda utajiri, afya, usalama, faraja, kushukuriwa na tunapenda mambo mengine mengi. Lakini Mungu anaagiza tuyakatae mambo haya tunapokuwa na nafasi ya kujitoa ili tumsaidie mtu mwingine kwa upendo (Flp 2:3-5). Kujitwika msalaba na kumfuata Yesu ni kusema ndiyo kwa mapenzi yake. Kwa mfano ni kusaidia wajane na yatima, ni kutangaza Habari Njema ya Mungu, ni kuwatendea watu haki, ni kufuata agizo lo lote la Biblia linalotulenga. kujikatalia na kumwambia Yesu ndiyo, yote ni kujitoa. Kujitoa ina gharama na ndiyo sababu Yesu anaifananisha na kubeba msabala. Mungu anataka tujitoe kwake kama sadaka (Rum 12:1-2)

a. Kwa ajili ya kutangaza Habari Njema ya Kristo po pote duniani, tunaweza kujitoa kama sadaka kwa njia zipi?

b. Namna gani tunaweza kujitoa katika familia zetu. Zaidi katika ndoa zetu?

c. Unafikiri kwamba viongozi wa kanisa wanapaswa kujitoa? Wanaweza kujitoa namna zipi?

Katika mstari wa 3:17 mtume Yohana anaendelea kutupatia mfano halisi wa namna tunavyoweza kuonesha upendo wetu kwa wengine. Ikiwa muumini mmoja mwenye uwezo anamwona muumini mwenzake ana mahitaji, ni wajibu wake kufanya nini? Kuna jibu moja tu: anapaswa kumsaidia. Hapa ni ukristo wa kweli wenye maana. Yohana anatusihi kuwatendea wenzetu wenye shida kwa upendo.

d. Je, wewe, unaweza kupatambua mahali (sehemu) fulani katika maisha yako ambapo unaweza kuutumia upendo wa namna hii? Andika hapo chini:

Maneno ya mwisho ya Yohana katika mistari hii ni muhimu. *"Watoto wadogo, tusipende kwa neno, wala kwa ulimi, bali kwa tendo na kweli"* (3:18). Upendo hauoneshwi kwa kusema tu. Watu wasiomjua Kristo hawavutwi kwa Bwana Yesu kwa njia ya matamshi yetu tu, hata kama ni maneno yenye maana. Matendo ya upendo yanathibitisha maneno tunayoyasema na yanaufanya upendo wetu kuwa hai na wenye maana.

Upendo uliokamilika ndani ya muumini ni ishara

(2:5; 4:12,16-18)

Maneno "kamili," "kamilifu," na "kamilika" yanatajwa mara nne katika waraka wa kwanza ya Yohana na yanatumiwa kuelezea habari za upendo. Katika 1 Yohana 2:4,5 tunaona utiifu wa Mkristo ni ishara ya kwamba upendo wa Mungu umekamilika ndani yake, na upendo huo ni ishara ya kwamba Mkristo huyu yumo ndani ya Kristo – *"Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki amri zake, ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake. Lakini yeye alishikaye neno lake, katika huyo upendo wa Mungu umekamilika kweli kweli. Katika hili twajua ya kuwa tumo ndani yake."* Upendo wa Mungu unafanya kazi ndani ya muumini. Upendo wa Mungu unapokamilika ndani ya muumini huyu Mkristo atampenda Mungu na atataka kumpendeza na kuzitii amri zake. Upendo mkamilifu unaonekana katika kutii, tena upendo unamwezesha Mkristo kutii. Huu ndio uzuri wa upendo.

Tena katika 1 Yohana 4:12, tunaambiwa, *"Pendo lake limekamilika ndani yetu"* kwa sababu, *"Mungu hukaa ndani yetu."* Yaani, tendo letu la kumpenda Mungu na kupendana ni ishara inayothibitisha tumeokoka kweli na Mungu amekaa ndani yetu kweli kweli. Katika mwanzo wa mstari huu tunasoma kwamba, *"Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote."* Ijapokuwa haiwezekani kwetu kumwona Mungu kwa macho yetu, tunaweza kuwa na uhakika kwamba Bwana Mungu anakaa ndani yetu ikiwa tunapendana. Tendo la kupendana linaonesha upendo wa Mungu umekamilika ndani yetu. Wakati upendo wa Mungu ulio ndani yetu unatufanya kuwa watu wa upendo na wenye kujitoa, ndipo upendo wa Mungu unafikia utimilifu wa kusudi lake.

1 Yohana 4:16-18 inasema tena, upendo wetu ni ishara ya kwamba tumekaa ndani ya Mungu na Mungu amekaa ndani yetu (Yn 17:26). Upendo wa Mungu unakamilika ndani yetu pale ambapo sisi wenyewe tunapendana. Tunapoona jinsi tunavyompenda Mungu na jinsi tunavyopendana, tunapata ujasiri wa kufikia siku ya hukumu bila hofu, maana upendo ulio ndani yetu ni uthibitisho wa kwamba sisi ni wa Mungu na hivyo hatutahukumiwa na kutupwa katika ziwa la moto. Yaani, upendo wa Mungu ni mkamilifu, na wakati upendo mkamilifu unapotawala maisha ya mtu, hofu yote inaondolewa. 1 Yohana 4:18 inatuonesha kwamba haiwezekani kwa upendo na hofu kuishi kwa pamoja ndani ya mtu. Mkristo anayeishi chini ya utawala wa Roho Mtakatifu hawezi kuwa na hofu ya kuhukumiwa wakati thawabu zitakapotolewa katika Kiti cha Hukumu cha Kristo. Wakati upendo unapotawala maisha ya muumini, hakuna kitu kitakachomletea hofu.

Kipi kinafurahisha, kumtumikia Mungu au mwingine? Tunaweza kusema pamoja na mtume Paulo, *"upendo wa Kristo watubidisha"* (2 Kor 5:14)?

<u>Maana Kwetu Leo</u>

1. Maana ya upendo ni nini?

2. Jambo gani lingetokea kama wote wanaojiita "Wakristo" wangependana kikamilifu?

3. Wakati Mkristo anapomkosea mwenzake, je, anapaswa kumwendea na kumwomba msamaha?

a. Eleza kama wewe umewahi kufanya hivyo. Je, mambo yalikuwaje?

b. Onesha mfano kutoka katika Biblia.

4. Wakati sisi tunapotendewa vibaya, tunapaswa kuonesha upendo kwa kumsamehe yule aliyetukosea?

a. Eleza kama wewe umewahi kufanya hivyo. Je ilikuwaje?

b. Onesha mfano kutoka katika Biblia.

5. Ni kitu gani kinachomfanya mtu kuwa mdanganyifu moyoni mwake? (1 Yn 3:17-18)

6. Maana ya "tusipende dunia" ni nini? (1 Yn 2:15)

Mistari Mikuu

1 Yohana 3:16, 18 – "Katika hili tumelifahamu pendo, kwa kuwa yeye aliutoa uhai wake kwa ajili yetu; imetupasa na sisi kuutoa uhai wetu kwa ajili ya hao ndugu . . . Watoto wadogo, tusipende kwa neno, wala kwa ulimi, bali kwa tendo na kweli."

FUNDISHO #7 - KUWAPA WAKRISTO UHAKIKA WA WOKOVU

Hili ni kusudi la saba la kuandikwa kwa waraka wa 1 Yohana. Yohana alitaka Wakristo kuwa na hakika kwamba wameokoka akisema kwamba uthibitisho wa wokovu huo unaonekana katika mabadiliko kwenye maisha yao.

Yohana aliandika mambo haya kwa sababu katika karne ya kwanza kulitokea kundi au chama cha watu wenye kiburi waliojidai kuwa na akili nyingi kuliko Wakristo wenzao hasa kuhusu mambo ya Mungu na kiroho. Walijiita "Gnostics" au wenye akili au kufahamu, wakidhani kwamba wao wenyewe walikuwa na akili maalum. Si kwamba walisema wamepata maarifa yao kutoka Biblia wala kutoka kwa Mungu, bali walidai chanzo cha maarifa yao kilikuwa kitu cha siri kilichotokana na uzoefu wao wa mambo ya kiroho. Waliona wao wenyewe walikuwa wenye "kujua" mambo ya kiroho kuliko wengine. Karibu barua nzima ya Yohana ni yenye kusudi la kupigana na mawazo mbalimbali ya walimu hawa wa uongo kama tulivyoonesha katika mwanzo wa kitabu hicho.

Kwa mfano, Gnostics hawa walifundisha kwamba vitu katika dunia hii ni vyenye uovu katika asili yake wakati vitu vilivyo vyema ni vya roho tu. Ina maana, katika mawazo yao, yale ya roho yanatenganishwa na yale ya dunia na moja haiingilii nyingine wala kuathiri nyingine. Kutokana na imani hiyo waliamini miili ya watu ni miovu tu, lakini uovu wa miili ya watu haukuweza kuathiri au kudhuru roho za watu na mambo yao ya kiroho. Maarifa haya ya uongo yaliwafanya kuamini Mkristo anaweza kutenda dhambi na uovu bila kuathiri maisha yake ya kiroho kwa kuwa ni vitu viwili visivyoingiliana.

Mbaya zaidi, walimu wa kundi hilo walikuwa wakiichafua habari ya Injili. Kwanza walisema Yesu hakuwa mwanadamu na wala hakuvaa mwili wa ubinadamu kwa kuwa miili ni miovu. Walidai Yesu ni roho tu na alionekana kuwa na mwili wakati hakuwa nao kweli. Isitoshe, walidai kabla Yesu hajafa msalabani, roho yake, ambayo ndiye yeye mwenyewe, iliondoka na kuacha mwili ule, usio wa kweli, kufa msalabani. Ndiyo kusema walifundisha

Yesu hakufa msalabani kwa ajili ya dhambi za wanadamu. Ndiyo sababu Yohana alikaza wazo la kwamba yeye mwenyewe alishuhudia mwili wa Yesu, alimwona kwa macho yake, alimsikiliza maneno yake, na alimshika kwa mikono yake (1 Jn 1:1-3; Jn 1:14). Yohana alijua ilikuwa lazima Yesu awe binadamu ama sivyo asingeweza kufa kwa ajili ya dhambi za wanadamu.

Kwa walimu hawa wa uongo, wokovu haukupatikana katika kusamehewa dhambi kupitia msalaba. Kwanza walifikiri hawakuhitaji msamaha kwa kuwa dhambi za miili yao yenye uovu hazikuwa na maana yo yote katika maisha yao ya kiroho. Badala yake, waliamini wokovu unapatikana katika kuongeza maarifa. Walifikiri mtu anahitaji kuongeza uelewa wake wa mambo ya kiroho tu, yaani, aelewe mambo ya uovu hayaingiliani na mambo ya kiroho. Hawakuhitaji kuokolewa na dhambi bali walihitaji kuokolewa na hali ya kutokuwa na maarifa yaliyo sahihi; yaani walihitaji kuokolewa na hali ya giza katika akili zao tu.

Mafundisho na maarifa haya maalum yalikuwa yakiwapa Wakristo wa kweli wasiwasi kuhusu imani yao. Ndiyo maana Yohana aliwaandikia akitaka kuwahakikishia kwamba imani yao ni ya kweli na imani ya walimu hawa ni ya uongo. Alitaka wajue ukweli wa dhambi na hitaji la wanadamu kusamehewa dhambi zao. Alitaka wafahamu kwamba kweli Yesu alikuwa 100% Mungu na 100% mwanadamu wakati moja na kwamba kweli alikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zao. Yaani, alitaka wafahamu wameokoka kweli na ndiyo maana alitaka watambue mabadiliko katika maisha yao kuwa ishara au uthibitisho wa wokovu huo. Kwa mfano alitaka waone hawakuwa watiifu kabla hawajaokoka lakini sasa wamekuwa watiifu na mabadiliko haya ni uthibitisho wa wokovu wao. Au, kama tulivyoona, alitaka waone kupendana kwao kuwa uthibitisho wa wokovu uliowabadilisha.

Roho Mtakatifu aliyajibu mafundisho hayo ya uongo kwa kumwongoza Yohana kuandika katika barua hii maarifa ya Mungu yaliyo kweli. Roho Mtakatifu alimwongoza Yohana aandike kuhusu mada hiyo kwa kuwa kila Mkristo anahitaji kuwa na uhakika kwamba ameokoka na ana uzima wa milele.

Tulishaona kwamba katika barua hii kuna maneno fulani yanayotajwa mara kwa mara. Moja ya maneno haya ni neno “Kujua”. Maneno yenye maana ya “kujua” yanatajwa zaidi ya mara thelathini na tano katika 1 Yohana. Yohana anataja maneno kama haya mara nyingi kwa sababu alikuwa akipigana na uongo wa Gnostics wale ambao walijidai kuwa wenye maarifa maalum kuhusu mambo ya kiroho. Yohana anataka kuonesha maarifa yao ni ya uongo na maarifa ambayo yeye alipewa na Mungu ni ya kweli.

Injili ya Yohana iliandikwa kusudi watu wapate kumwamini Yesu Kristo na kuokolewa (20:31). Kusudi hilo hilo ni kusudi moja la waraka wa kwanza ya Yohana lakini muhimu zaidi, katika 1 Yohana, ni kusudi la Yohana kuwapa wasomaji wake uhakika kuhusu wokovu walio nao tayari. Katika 1 Yohana 5:13 tunasoma kwamba barua hii iliandikwa *“ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele.”* Kusudi la Yohana si kwa wasomaji wake kuamini na kupokea uzima wa milele tu, bali anataka wawe na uhakika kwamba walishaokoka kweli kweli hata milele.

Katika Kiyunani kuna maneno mawili yenye maana ya “kujua”. Moja ina maana ya maendeleo katika akili. Neno la pili lina maana ya ukamilifu wa akili, au kuwa na hakika kabisa bila mashaka. Imani katika Kristo Yesu iletayo wokovu inampa muumini uhakika wa kwamba ameokoka.

a. Mtoto wa Mungu anaweza kuwa na uhakika na mambo gani yaliyo katika mistari ifuatayo:

2 Tim 1:12 -

Rum 8:28 –

2 Kor 5:1 –

Kila Mkristo ajipime mwenyewe ili awe na uhakika wa wokovu wake

Katika 2 Wakorintho 13:5, Paulo anasema, *"Jijaribuni wenyewe kwamba mmekuwa katika imani; jithibitisheni wenyewe. Au hamjijui wenyewe, kwamba Yesu Kristo yu ndani yenu? "* Kila Mkristo anapaswa kuyatumia maelezo ya Biblia kujichunguza na kuhakikisha ameamini kweli kweli na kuokoka. Inawezekana kwa mtu kujiita Mkristo wakati yeye siyo Mkristo wa kweli. Yaani, mtu huyu atakuwa amejidanganya au pengine anajijua lakini kusudi lake ni kuwadanganya wengine. Kwa sababu hiyo Yohana anasema watu kama hawa, *"Walitoka kwetu, lakini hawakuwa wa kwetu. Maana kama wangalikuwa wa kwetu, wangalikaa pamoja nasi. Lakini walitoka ili wafunuliwe kwamba si wote walio wa kwetu"* (2:19).

Basi tuchunguze vizuri 1 Yohana 5:1-5 na kutambua mambo yanayoonesha kwamba mtu ana imani ya kweli. Imani ya kweli ni nini? Imani ya kweli ni imani inayookoa na inajulikana kwa matunda yake yaliyo katika maisha ya Mkristo. Ni imani inayoonekana, yenye kutumika, na yenye ushindi.

1 Yohana 5:1-5 – "Kila mtu aaminiye kwamba Yesu ni Kristo amezaliwa na Mungu. Na kila mtu ampendaye mwenye kuzaa, ampenda hata yeye aliyezaliwa na yeye. Katika hili tunajua kwamba tunawapenda watoto wa Mungu, tumpendapo Mungu, na kuzishika amri zake. Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake; wala amri zake si nzito. Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu; na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu. Mwenye kuushinda ulimwengu ni nani, isipokuwa ni yeye aaminiye ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu?"

Uhakika wa wokovu unapatikana katika kuelewa imani inayookoa ni zawadi kutoka kwa Mungu

Je, umetambua ukweli wa kwamba kupata kuwa muumini ni jambo la kupewa? Imani ni karama au zawadi kutoka kwa Mungu. Watu wengi wanawaza kwamba kuwa Mkristo ni jambo la kushinda masomo fulani. Wanaamini ni juu ya mtu kujitayarisha na akifikia kipimo fulani katika uelewa wake atafaa kuwa muumini. Ijapokuwa hili ni wazo la baadhi ya watu, wazo hilo siyo la kweli.

Kuamini kunaanza kwa kuupokea msaada wa Mungu. Kuwa Mkristo si lazima tujikaze kufikia kipimo fulani. Mungu anatupokea kama tulivyo - wenye dhambi. Katika Injili ya Yohana tunasoma kwamba, *"Wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu"* (1:12). Si jambo gumu kuzaliwa na Mungu. Ni Mungu anayelifanya tendo lile na atalifanya kwa ye yote anayekuja kwake kwa njia ya Yesu Kristo.

Wakristo wengine wana mashaka na wokovu wao kwa sababu wanafikiri wokovu unapatikana kupitia jitihada zao badala ya kuwa ni zawadi kutoka kwa Mungu. Wasiwasi unaowapata hutokana na kufikiri labda hawajajitahidi vya kutosha. Hasa wanapotenda dhambi wanaona jitihada zao zimepungukiwa. Lakini, wangeelewa kwamba imani yao, na hata wokovu wao, ni zawadi ya Mungu kutokana na neema yake, wangepumzisha mioyo yao wakijua wokovu wao unamtegemea Mungu na siyo jitihada zao.

Uhakika wa wokovu unapatikana katika uamuzi wa kumwamini Yesu

Imani katika Kristo inayotuokoa na inayotupatia uzima wa milele, si imani ya akili kana kwamba ni maarifa ya kujua tu. Bali ni uamuzi katika moyo wa mtu akiamua kumtegemea Yesu kulingana na habari alizojifunza juu yake. Tunapaswa kukumbuka kwamba imani inayookoa haipati msingi wake katika ufahamu wa mtu peke yake. Kuna watu wengi wanaoamini habari ya Yesu kama vile wanavyoamini habari juu ya watu wengine wakubwa katika historia. Wanaamini kwamba Yesu alikuwa mtu hakika katika historia lakini hawamtegemei kwa imani inayookoa. Imani yao ni ya akili tu. Ikiwa imani ya mtu ni ya ufahamu na akili tu, basi Biblia inafundisha kwamba imani ile imekufa.

Lakini Yohana anasema, *"Kila mtu aaminiye kwamba Yesu ni Kristo amezaliwa na Mungu" na "Mwenye kuushinda ulimwengu ni nani, isipokuwa ni yeye aaminiye ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu?"* Yohana anataka wasomaji wake kujiuliza kama wamemwamini Yesu au la. Kama wamemwamini Yesu, Yohana anasema ni kipimo mojawapo kinachothibitisha kuokoka kwao. Ni kama anawauliza, "Je, unaamini Yesu ni mwana wa Mungu na kwamba

alikufa kwa ajili ya dhambi zako?" Wanapojibu ndiyo anasema, "Basi, mjue mmeokoka kweli kweli."

Uhakika wa wokovu unapatikana katika imani inayodumu

Jambo lingine tunalopaswa kujua ni kwamba imani inayookoa ni imani inayodumu. Yesu aliongea imani isiyodumu katika Mathayo 13:5-6, *"Nyingine zikaanguka penye miamba, pasipokuwa na udongo mwingi; mara zikaota, kwa udongo kukosa kina; na jua lilipozuka ziliungua; na kwa kuwa hazina mizizi zikanyauka."* Imani isiyodumu, wala siyo imani. Ni hali ya kuwadanganya wengine kwa kuwaiga wale wenye imani ya kweli. Kwa sababu kiigizo hiki hakidumu kinaonesha kwamba kile kilichofanana na imani hakikuwa imani kweli. Ndiyo maana Yohana anasema wengine "w*alitoka kwetu, lakini hawakuwa wa kwetu. Maana kama wangalikuwa wa kwetu, wangalikaa pamoja nasi. Lakini walitoka ili wafunuliwe kwamba si wote walio wa kwetu"* (2:19).

Uthibitisho mwingine wa kwamba Mkristo ameokoka kweli ni jinsi anavyodumu katika imani yake. Kwa mawazo ya Yohana, wengine wanaoacha kujiita Wakristo njiani hawakuwahi kuwa Wakristo wenye imani. Maana, wangekuwa Wakristo kweli wangedumu katika imani yao. Yohana anataka wasomaji wake kushuhudia jinsi wanavyoendelea katika imani yao. Wakishatambua hivyo, Yohana anataka waelewe kwamba ni uthibitisho mojawapo wa kwamba wameokoka kweli na wana uzima wa milele.

Uhakika wa wokovu unapatikana katika upendo wa Mkristo

Katika 1 Yohana 5:1-2, imani ya kweli ina matunda ya kumpenda Mungu Baba na kupendana kati ya Wakristo. Upendo wa Mungu ulioneshwa na tendo la Mungu kumtuma Mwana wake wa pekee duniani kwa ajili yetu. Tunapopokea upendo wa Mungu, na kuokoka kwa njia ya kumwamini Yesu Kristo, matunda ya imani au wokovu huo yanaonekana kwa jinsi tunavyoanza kumpenda Mungu na kuwapenda Wakristo wenzetu. Tunampenda Mungu kwa sababu yeye alitupenda kwanza. Tunaonesha upendo wetu kwa Mungu kwa njia ya matendo ya upendo yanayoonekana. Kwa mfano upendo wetu unaonekana wakati tunalitii Neno lake na vilevile wakati tunapowasiliana naye (kuomba) na hata kwa njia zingine kama kujitoa kwake, kumtumikia n.k. Tunawapenda ndugu zetu kwa sababu Mungu ametuamuru kufanya hivyo. Upendo huo pia unaonekana katika matendo yetu. Kwa mfano, unaonekana wakati tunasaidiana, tunatiana moyo, tunapojengana n.k. Imani yetu ya kweli iliyotuokoa inaonekana katika matendo haya ya kumpenda Mungu na kupendana sisi kwa sisi. Soma 1 Yohana 3:1,11,16,23; 4:7,11,20.

Yohana anataka wasomaji wake kujichunguza kuona kama wanampenda Mungu na pia kama wanapendana. Pale wanapokuta kuna upendo mioyoni mwao, Yohana anasema ni uthibitisho wa kwamba wameokoka na wana uzima wa milele.

Uhakika wa wokovu unapatikana katika utiifu wa Mkristo

Imani ya kweli inajulikana pia katika jinsi mtu anavyomtii Mungu baada ya kuokoka. Ikiwa uhusiano wetu na Mungu ni uhusiano wa kweli, basi tutakuwa watu wanaotii Neno lake. Kama tulivyosema tayari, utiifu wetu ni namna moja ambayo upendo wetu kwa ajili ya Mungu utaonekana. Tena, utiifu huo, utakuwa uthibitisho wa kwamba tumeamini kweli na kuokoka. Yaani, mtu anaweza kujipima katika utiifu wake ili ajue kama ameokoka au la. Si kwamba ni lazima mtu aweze kumtii Mungu asilimia mia bila kutenda dhambi yo yote (kwa kuwa hali hii haiwezekani). Bali, mtu anapopima alivyotii kabla hajaokoka na jinsi anavyotii baada ya kuokoka, lazima aweze kuona mabadiliko na maendeleo katika kumtii Mungu yanayotokana na nia na hamu mpya zake za kutaka kumtii Mungu.

Uhakika wa wokovu unapatikana katika ushindi wa Mkristo

Imani inayookoa haimkubali Kristo ili kupewa wokovu na kwenda mbinguni tu, bali inamkubali Kristo ili Mkristo ashinde maishani mwake hapa hapa duniani. Mara tatu Yohana anatumia maneno ya kusema Mkristo anaishinda dunia (5:4-5). Mtume Yohana anasema, "*Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu."* Anaeleza kwamba

kushinda huku si kwa sababu ya kuzaliwa kwake, bali kwa sababu ya imani yake. Neno linalotumiwa hapa ni lenye kuonesha ushindi unaoendelea katika maisha ya Mkristo. Ndiyo kusema Mkristo anayeendelea kuwa na imani ataendelea kushinda. Ushindi katika Kristo ni hali ya kuyatimiza mapenzi ya Mungu na kutoruhusu dhambi kututawala. Ishara ya ushindi inaonekana katika mambo mengi kama vile tunda la roho maishani mwa Mkristo (Gal 5:22-23).

Yohana anasema kwa wasomaji wake, "Kuna dalili za kushinda katika maisha yako ya Kikristo?" Anataka watambue jinsi wanavyoshinda na katika hilo wajue ni uthibitisho mwingine wa kwamba wameokoka kweli na wanao uzima wa milele.

a. Tofauti ya Mkristo na dunia ni nini? Maandiko haya yanatusaidia kujibu swali hilo (1 Yn 2:15-17; Yn 12:31; 14:30; 16:11; 2 Kor 4:4).

b. Sisi tunaishi katika dunia iliyo adui yetu. Tunawezaje kuishinda dunia hii?

Yesu Kristo ni msingi wetu. 1 Yohana 4:4 inasema, *"Ninyi, watoto wadogo, mwatokana na Mungu; nanyi mmewashinda, kwa sababu yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia"* Tuna hakika kwamba tutaishinda dunia kwa njia ya Yesu Kristo Mwokozi wetu. Imani yetu ipo katika Mwokozi aliyeyashinda mambo yote, na sisi tunahakikishiwa tutashinda kwa sababu yeye alishaishinda dhambi, mauti, na Shetani.

Imani inayookoa inahitajika kwa kila mtu

Imani ya kweli ni ya pekee kwa sababu ni jambo lililo kati yako na Mungu. Hakuna mtu mwingine anayeweza kukukatia shauri la kumpokea Bwana Yesu. Ni Imani yako binafsi kwa kuwa ni lazima wewe mwenyewe uweke imani yako katika Kristo peke yake na katika kazi ile kubwa alioifanya msalabani.

<u>Maana Kwetu Leo</u>

1. Ikiwa una mashaka au hofu kuhusu mahali utakapoenda baada ya kufa, unapaswa kufanya nini?

2. Kuna tofauti gani kati ya kukubali kwa akili tu na imani inayookoa? (1 Yn 2:3-5)

3. Namna gani tunaweza kuwa na hakika kwamba sisi tumo ndani ya Yesu? (1 Yn 2:5,29)

4. Kuna alama au ishara inayofuta mashaka na ambayo inathibitisha kwamba mtu amezaliwa na Mungu? (1 Yn 4:14; Linganisha 1 Yn 3:14 na Mt 5:21-22)

5. Kama Roho Mtakatifu hakai ndani ya mtu, je, inawezekana kwa mtu yule kuwa Mkristo? (Rum 8:9,16; 1 Kor 3:16; 6:19-22; 1 Yn 3:14; 4:13)

Mistari Mikuu

1 Yohana 5:10-13 – "Yeye amwaminiye Mwana wa Mungu anao huo ushuhuda ndani yake. Asiyemwamini Mungu amemfanya kuwa mwongo, kwa kuwa hakuuamini huo ushuhuda ambao Mungu amemshuhudia Mwanawe. Na huu ndio ushuhuda, ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo katika Mwanawe. Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima. Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele, ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu."

MWISHO

Sisi viongozi wa makanisa tunapaswa kujifunza Neno la Mungu tukiwa na makusudi makubwa mawili:

1. Kusudi la kwanza ni kujiendeleza katika maisha yetu ya kiroho kwa maana Neno la Mungu ni chakula kwa mioyo yetu.
2. Kusudi la pili ni kumwelewa Mungu zaidi ili tuwe na uwezo, kama viongozi, kuwalisha Wakristo walio mikononi mwetu.

Kwa sababu umeshajifunza na kusaidiwa mwenyewe katika moyo wako, sasa uwasaidie Wakristo wengine kwa kuwafundisha maneno uliyojifunza. Kumbuka kwamba wewe ni kama mama anayelisha mtoto wake. Kinywa cha mtoto na kinywa cha mama ni tofauti. Kwa sababu hii usijaribu kuwalisha Wakristo wachanga kwa kipimo kilicho kikubwa kuliko uwezo wao wa kumeza. Uwasaidie kulifahamu Neno la Mungu na kulitumia katika maisha na mwenendo wao. Mungu awasaidie na awabariki katika kazi hii.